# Nipashe

Jumatano Desemba 20, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581530

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**MABASI** kupewa wakala, chanzo ajali zisizoisha



UKURASA 5

**JWTZ** yapeleka askari wake 300 kulinda amani Afrika ya Kati

UKURASA 5

**UCHAGUZI DRC;** Wagombea urais 18 yumo mama pekee, jeshi lasimamia vifaa

UKURASA 19




UKURASA 11

## UTAFITI MPYA

# Tiba antibaiotiki janga kwa watoto

**YAPATIWA** mbadala rasmi kunusuru kizazi...*Endelea ukurasa 2*



UKURASA WA 24

## SIMBA SC WAWAWAAAH!

MABAO mawili ya Mcameroon Willy Onana, jana yalifufua matumaini ya Simba kutinga kwa mara nyingine tena robo fainali



## Viongozi wa dini wataka fedha migodi zisaidie bima mpya afya

UKURASA 3

## Mbaroni na simu 305, laptop 10 za kudhalilisha wanawake

UKURASA 2

**MICHEZO** GAMONDI: NI USHINDI TU LEO UK. 23

**KATUNI** UK. 6

# Antibaiotiki janga kwa watoto

**Na Jenifer Gilla**

WATAFITI kutoka Taasisi ya Afya Ifakara (IHI) na Swiss Tropical and Public (Swiss-TPH) wamegundua vifaa vya kidijitali vyenye uwezo wa kuonesha ugonjwa halisi anaoumwa mtoto na kumsaidia daktari kutoa dawa kulingana na ugonjwa uliogundulika.

Lengo la kutumika kifaa hicho ni kupunguza matumizi ya dawa za antibaiotiki kwa watoto ambayo wakati mwingine huandikiwa na madaktari kwa kuangalia dalili zilizopo baada ya vipimo kushindwa kuonesha tatizo linalomsumbua.

Mtafiti na mwandishi wa utafiti huo kutoka IHI, Dk. Lameck Luwanda, alisema jana kuwa kupitia kipimo hicho watapiga hatua kubwa kupunguza matumizi ya dawa hizo na kuokoa maisha ya watoto wengi.

Alisema vipimo vya kawaida vinavyotumika sasa, havina uwezo wa kuona magonjwa yote ya watoto, hivyo daktari analazimika kuandika dawa zikiwamo za antibaiotiki kwa kuangalia dalili alizonazo mgonjwa.

Alisema kipimo hicho kimetengenezwa kwa teknolojia ya hali ya juu yenye uwezo wa kumpima mtoto na kugundua ugonjwa halisi unaomsumbua, hivyo kumsaidia daktari kutoa dawa kulingana na tatizo lililopo badala ya kutoa dawa jumuishi.

Alisema msukumo wa kufanya utafiti wa kipimo hicho ulitokana na utafiti wa kisayansi unaoonesha kuwa vifo milioni 1.2 vilivyotokea mwaka 2019, vilihusishwa na matumizi ya dawa hizo huku idadi kubwa zaidi ya wagonjwa ikitoka Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alisema utafiti huo ulifanyika Tanzania kwa miaka mitano kama sehemu ya mradi wa DYNAMIC na kuongozwa na Kitengo cha Kidijitali na 'Global Health' cha Unisante, kwa ushirikiano na washirika kadhaa.

Utafiti huo ulishirikisha vituo vya afya 20 nchini katika kipindi cha miezi 11.

Kwa mujibu wa Dk. Luwanda, katika hospitali zilizotumia kipimo hicho, dawa za antibaiotiki zilitolewa kwa asilimia 23.2 kulinganishwa na asilimia 70.1 katika vituo vingine 20 vya afya ambako chombo hicho hakikutumika.

Katika utafiti huo, wanasayansi waligundua kuwa kutumia kipimo hicho cha kidijitali kulipunguza kwa kiasi kikubwa kuwapa watoto dawa za antibaiotiki bila kuathiri matokeo ya kliniki.

Hata hivyo, watafiti hao wanabainisha kuwa utafiti huo unawakilisha suluhu inayoweza kupanuka kulingana na gharama na teknolojia, ili kupunguza kuagiza dawa hizo kwa usalama wa watoto.

Dk. Leah Rwezaula, Ofisa wa Kliniki na Daktari anayesimamia Zahanati ya Iganzo, akitumia zana hiyo ya kidijitali, alisema kupitia zana hizo ameongeza uelewa wa namna bora ya kuhudumia wagonjwa.

"Kutumia kipimo hiki sasa hata mtoto akija, ninaweza kugundua tatizo halisi linalomsumbua na kumwandikia dawa sahihi tofauti na hapo nyuma, kipimo kikionyesha hakuna ugonjwa, nilikuwa ninamwandikia dawa kwa kuangalia dalili," alisema.

Mradi wa DYNAMIC umetekelezwa kwa ushirikiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na Uswisi, ili kusaidia kuboresha ubora wa huduma na kupunguza matumizi ya dawa za antibaiotiki.

Kwa sasa kipimo hicho kimesambazwa katika vituo vya afya zaidi ya 100 vya Tanzania na Rwanda.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
20.12.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya **Alhamisi tarehe 21-12-2023 hadi tarehe 23-12-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero** kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 453 DYG / T 572 EAZ T 853 DXS / T 568 EAZ T 319 EDD / T 394 DVS T 988 EDR / T 394 DVS T 162 DFC / T 393 DVS**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu** - **mita 24.00**
**Upana** - **mita 4.80**
**Kimo** - **mita 5.20**

3. Njia itakayotumika: ***Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero*** kupitia ***Mikumi,*** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akipokea zawadi maalum kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, katika hafla ya maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**


MKOMBOZI COMMERCIAL BANK
a bank with integrity

**MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUHAMA KWA MAKAO MAKUU**

Tunapenda kuwataarifu wateja na wadau wetu wa thamani kuwa, Makao Makuu ya Benki ya Biashara Mkombozi yamehamia kwenye jengo jipya la St. Joseph House (gorofa ya chini, ya kwanza na ya pili) ya jengo hilo ambalo liko katika Ploti namba 40, Mtaa wa Mansfield, Nyuma ya Kanisa la Mtakatifu Yosefu.

Tafadhali kumbuka kuwa anuani na namba za simu hazijabadilika.

**Benki ya Biashara ya Mkombozi**
**Ploti Namba. 40. Mtaa wa Mansfield,**
**S.L.P 38448.**
**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Simu: +255 22 2137806/7**

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote ukaojitokeza.

**Imetolewa na**
**Menejimenti.**

217763901


# Mbaroni na simu 305, laptop 10 za kudhalilisha wanawake

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watu wawili wanaodaiwa kuwawekea wanawake dawa za kulewesha kisha kuwadhalilisha kingono, kuwaibia na kuwatishia kuwaua.

Vilevile, linawashikilia wengine watatu kwa tuhuma za wizi wa vifaa vya boti ambazo ni injini mbili aina ya Yamaha 200P, betri mbili za boti zenye thamani ya Sh. milioni 160.307.

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alibainisha hayo jana jijini, akifafanua kuwa watuhumiwa wa udhalilishaji wanawake ambao majina yao wameyahifadhi, wamekuwa wakitekeleza vitendo hivyo baada ya kuwatongoza.

"Operesheni kali maalum iliyoanza mwezi Septemba 2023 na inayoendelea, imewanasa watuhumiwa mbalimbali wakiwamo watu hawa wawili ambao huwatongoza wanawake, wanawawekea dawa za kulewesha kisha kuwafanyia vitendo vya udhalilishaji wa kingono na kuwapiga picha, kuwatishia kuwaua wakitoa siri za udhalilishaji huo na baadaye kuwaibia simu, laptop na fedha," alisema.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao wamekamatwa na laptop 10, simu za kiganjani 305 za aina mbalimbali, runinga 36, kamera nne, sabufa tatu na mifuko ya 160 ya simu.

Alisema baadhi ya vitu hivyo tayari vimetambuliwa na wamiliki wake na kwamba "watuhumiwa hao watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria".

Kuhusu wezi wa vifaa vya boti, Kamanda Muliro alisema pia wamekamatwa wakiwa na gari namba T 485 CWU aina ya Suzuki, mali ya Teusin Van Bauren, mfanyabiashara raia wa Afrika Kusini.

"Watuhumiwa hao ni Msabaha Michael (37) maarufu Askofu, mkazi wa Vikindu; Juma Athuman (45) maarufu Dito, mkazi wa Mbagala; na Joseph Januari (23), dereva na mkazi wa Tandale Kwatumbo.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi limejipanga vizuri kuhakikisha wananchi wanasherehekea kwa amani na usalama sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

HABARI KITAIFA

# Marekani yataja sababu kuirejesha Tanzania MCC

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani imetaja sababu za kuirejesha Tanzania katika Mfuko wa Changamoto za Milenia (MCC) baada ya kuiondoa miaka kadhaa iliyopita.

Mara ya mwisho MCC ilitoa msaada wa Dola za Marekani milioni 698 mwaka 2008 ambazo zilitumika hadi 2013.

Naibu Balozi wa Marekani nchini, Robert Raines, katika taarifa yake jana, alibainisha kuwa kuanzia 2008 hadi 2013, MCC ilishiriki katika uwekezaji wa kuboresha miundombinu ya barabara, nishati na maji Tanzania.

Alisema wanafarijika kwamba uteuzi wa Tanzania kwa mpango huo unatambua mageuzi ambayo yamefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tuna hakika kwamba mpango huu utasaidia mageuzi yanayoendelea, maendeleo ya kidemokrasia, utawala na utaimarisha ukuaji wa uchumi," alisema.

Alisema wanaamini programu hiyo itaunga mkono mageuzi yanayoendelea katika utawala wa kidemokrasia na itaimarisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini Tanzania.

Alisema Ubalozi wa Marekani unatarajia kufanya kazi kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania ili kuimarisha ukuaji uchumi na utawala wa kidemokrasia kwa manufaa ya Watanzania wote.

MCC hutoa fedha kama motisha kwa nchi ambayo inafuata demokrasia, uwazi, haki za binadamu na uhuru wa maoni.

**"Tuna hakika kwamba mpango huu utasaidia mageuzi yanayoendelea, maendeleo ya kidemokrasia, utawala na utaimarisha ukuaji wa uchumi," alisema.**

# Viongozi wa dini wataka fedha migodi zisaidie bima mpya afya

**Na Restuta James**

VIONGOZI wa dini wameishauri serikali kutunga kanuni rafiki zitakazowezesha utekelezaji rahisi wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kuongeza vyanzo vya mapato kutoka sekta za madini, mafuta na gesi katika kuchangia huduma za afya.

Mwenyekiti wa Kamati ya Dini Mbalimbali kuhusu Haki za Kiuchumi na Maadili ya Uumbaji, Askofu Nelson Kisare alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa sheria hiyo ni nzuri, lakini zisipotungwa kanuni bora, haitaleta tija iliyokusudiwa.

Alisema baadhi ya vyanzo vya mapato vya kugharamia matibabu kwa kaya maskini ni bahati nasibu, zawadi na misaada toka kwa marafiki, ambavyo alisema si vya uhakika.

"Sisi tulipokuwa tunapigania hii sheria tuliainisha hadi vyanzo vya mapato, sheria imetaja zawadi na bahati nasibu, hayo yasipokuwapo itakuwaje?" alihoji.

Askofu Kisare alisema serikali inapaswa kuangalia vyanzo vya uhakika ili kugharamia afya za Watanzania badala ya kutegemea misaada na zawadi ambazo hazijulikani kama zitakuja.

"Tumeshapata sheria, kazi iliyobakia ni kukikisha haikumbani na ukatili kupitia kwenye kanuni zitakazotungwa na waziri... serikali ibebe jukumu la afya za wanyonge, maskini na wazee.

"Kanuni hizi zitungwe katika msingi wa haki ambao unatambua utu na thamani ya Mtanzania ili tuwe na taifa ambalo watu wake wana afya nzuri... sisi viongozi wa dini tutaendelea kujadiliana na serikali ili tupate kanuni nzuri," alisema Askofu Kisare.

Mwenyekiti Mwenza wa kamati hiyo kutoka Baraza la Waislam Tanzania (BAKWATA), Sheikh Khamis Mataka, alisema viongozi wa dini walifanya utafiti na kupeleka mapendekezo serikalini, ambayo yamezaa sheria hiyo.

"Tunapoelekea katika utengenezaji kanuni, tunatamani kuona kila Mtanzania anafaidika kwa kufikiwa na huduma za afya... tunachokiangalia kwa sasa ni kuzidi kuiboresha ili kupitia kanuni kadi ya bima iwe suluhisho la kupata huduma za afya bila kikwazo," alisema.

Mshauri wa Masuala ya Kisheria wa kamati hiyo, Wakili Gloria Mafore, alisema moja ya vyanzo vya mapato vilivyopendekezwa na viongozi wa dini ni asilimia 0.01 ya kodi zinazotokana na madini, mafuta na gesi, ambacho ni chanzo cha uhakika kuliko bahati nasibu.

Aliishauri serikali kuweka mpango mzuri wa kusimamia ukwasi wa fedha za bima zinazopaswa kuwekwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ndani ya miaka miwili, ili zisitumike kugharamia huduma nyingine.

"Waziri anapotengeneza kanuni ni vyema wadau wakashirikishwa ili iwe rahisi kwa watu kuchangia na kuweka mazingira wezeshi ya vituo vya afya kutoa huduma kwa wananchi.

Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ulipitishwa rasmi na Bunge Novemba Mosi, mwaka huu na kutiwa saini na Rais Samia Suluhu Hassan Desemba 4, mwaka huu. Sasa ni sheria, lakini kanuni zake hazijatungwa.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) wakikagua mitambo ya kupozea umeme wa reli ya mwendokasi (SGR) katika kituo cha Pugu Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Wake wa viongozi wawafariji waathirika maporomoko Hanang'

**Na Mwandishi Wetu,** HANANG'

WAKE wa viongozi wa serikali kupitia kikundi chao cha Ladies of New Millennium Group, wametembelea maeneo yaliyoathiriwa na maafa yaliyotokea Desemba 3, mwaka huu wilayani Hanang', mkoani Manyara na baadaye kutoa misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa janga hilo.

Akizungumza baada ya kutembelea maeneo yaliyoathirika na kukabidhi misaada, Mkuu wa msafara huo, Mary Majaliwa alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa nguvu kubwa aliyoelekeza katika kuwasaidia waathirika wa maafa ili kuhakikisha maisha yao na maeneo yaliyoathiriwa yanarejea haraka katika hali ya kawaida.

"Tunapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia na serikali yake kwa juhudi kubwa zinazoendelea kufanyika katika mji wa Kateshi, lakini kwa upendo wake mkubwa kwa wananchi wa Hanang' na hata kukatisha ziara yake ya kikazi kwa ajili ya wananchi hawa," alisema.

Mary ambaye ni mke wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitoa wito kwa wananchi wa Hanang' na wale walioathirika na maafa kuwa na mshikamano katika kipindi hiki na kuwasisitiza kuendelea na shughuli zao na kuhakikisha watoto wao wanakwenda shule mara tu zitakapofunguliwa mwezi ujao.

Marina Juma, Mke wa Jaji Mkuu wa Tanzania, alitoa wito kwa kinamama wengine kuguswa na athari za maafa hayo na kujitolea chochote watakachoweza ili kusaidia waathirika wa maafa hayo.

Mke wa Hayati Rashid Kawawa, Asina Kawawa, alieleza kuguswa na namna Rais Samia alivyoshughulikia maafa ya Hanang'.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, baada ya kupokea misaada hiyo, alisema kuwa kwa sasa serikali inaendelea kurejesha mji wa Katesh na maeneo mengine yaliyoathirika katika hali yake ya kawaida ikiwamo miundombinu ya barabara, maji na pia kusaidia kutoa tope katika nyumba za watu.

"Wananchi wa Hanang' hususani maeneo ya Katesh, Gendabi na Jorodom wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia kwa msaada mkubwa ambao ameutoa," alisema.

Kundi hilo la New Millenium ambalo linaundwa na wake wa viongozi limetoa misaada mbalimbali ya kibinadamu kwa waathirka wa maafa, ikiwamo mabegi ya shule 250, viatu vya shule jozi 216, madaftari 500, madaftari makubwa 144, kalamu za risasi maboksi matano, sare za shule 200, nguo za ndani za watoto 600, fulana 170, kanga zaidi ya 100, vitenge 40, shuka 105 na mablanketi 125.

Vitu vingine ni mashati, magauni, suruali, mitandio, vyandarua, vyombo vya chakula na mchele kilo 450.

Maporomoko ya tope lililoambatana na mawe na magogo yalitokea Desemba 3, 2023 katika wilaya ya Hanang' na kusababisha vifo vya watu 89, majeruhi 139 na uharibifu wa nyumba, mali na miundombinu mbalimbali ya maji, umeme, barabara na pia kuathiri shughuli za kijamii na kiuchumi hususani katika mji wa Kateshi na vijiji vya Gendabi na Jorodom.

MAKALA MAALUM

# Nape arejea mkutano dunia, Tanzania ikifunguliwa milango zaidi mawasiliano

## •Neema simu, hali ya hewa, ndege, majini...

Na Rolf Kibaja



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Moses Nnauye, akizungumza na ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano Mkuu wa Masafa uliofanyika wiki iliyopita Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu. PICHA: MPIGAPICHA WETU

MSAMIATI 'masafa' katika mawasiliano ya kielektroniki, ina maana kubwa kwamba ndio nyenzo ya kufanikisha huduma kama vile mawasiliano ya simu, utangazaji wa redio na televisheni, intaneti, kuongoza safari za ndege na usalama wa anga.

Mengine ni uongozaji safari za vyombo vya usafiri majini na usalama wake, utabiri wa hali ya hewa, kukusanya taarifa kupitia satelaite angani, pia utafiti wa miamba yenye raslimali madini. Zote ni huduma zinazopatikana, kupitia msaada wa rasilimali masafa.

Kanuni za matumizi yake, pale inapokosewa, hugonganisha watumiaji wa eneo, hivyo, masafa hupangwa, kutokana na mahitaji na matumizi yake.

Katika kufanya kazi ya kupanga masafa na matumizi yake, ni jukumu linalorejewa na mkutano mkuu unaohusisha nchi zote duniani, kila baada ya miaka mitatu au minne.

**KINACHOJIRI MWAKA HUU**

Hivi karibuni, Tanzania imeshiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Upangaji wa Masafa ya Mawasiliano na Obiti za Satelaiti (World Radiocommunication Conference - WRC-23) uliofanyika jijini Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kuanzia Novemba 20 hadi tarehe 15 mwezi huu.

Ni mkutano ulioratibiwa na Shirika la Kimataifa la Mawasiliano Duniani. Kawaida yake, hufanyika baada ya tafiti mbalimbali zinazojadiliwa kiufundi na kuuwezesha kufanyika uamuzi katika kupanga masafa.

Mkutano uliopita ulijadili mada 40, zote ni muhimu kwa kila nchi, ukijikita katika kurejea upangaji wa masafa ya mawasiliano ya simu, usafiri majini na usalama wake, uongozaji ndege na usalama wa anga.

Kuna mengine yanayogusa utabiri wa hali ya hewa, mawasiliano katika kutabiri na kugundua majanga ya hatari, utangazaji televisheni, mawasiliano ya simu na intaneti, masafa kwa ajili ya matumizi ya rada na ukusanyaji taarifa kupitia obiti za satelite.

Vilevile, kuna suala la upangaji masafa uliotumia kanuni muhimu kila nchi kuwa na haki sawa katika upatikanaji masafa na obiti za satelaiti kwa mujibu wa Katiba ya Shirika la Kimataifa la Mawasiliano Duniani.

**TIMU YA TANZANIA**

Katika mkutano huo, ujumbe wa Tanzania uliundwa na wataalamu kwenye fani husika na uliongozwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

Akizungumza na ujumbe wa Tanzania katika kikao-kazi, baada ya kuhitimisha mkutano mkuu, Waziri Nape akasema Tanzania imeshiriki mkutano huo, ili kuhakikisha maslahi ya nchi yanatetewa katika upangaji wa masafa ya mawasiliano na obiti za satelaiti.

Ujumbe wa Tanzania pia ulikuwa na Balozi wa Tanzania katika Umoja wa Falme za Kiarabu, Luteni Jenerali, Yacub Mohammed, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Selestine Kakele na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Dk. Jabiri Bakari.

Nape akafafanua: "Tanzania inatekeleza mageuzi makubwa katika sekta ya mawasiliano, hivyo ni muhimu kwa nchi yetu kushiriki kikamilifu kwenye mkutano huu ili kuhakikisha kuwa masilahi yetu yanatetewa katika upangaji wa masafa ya mawasiliano na obiti za satelaiti, ili Tanzania iendelee kupiga hatua na kuwaletea wananchi maendeleo."

> **Wengine ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Watoa Huduma za Mawasiliano (MNOs), Ofisi ya Rais (PO), Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Chuo Kikuu cha Dar-Es- Salaam (UDSM), Taasisi ya Teknolojia ya Dar Es-Salaam (DIT).**

Nape akasisitiza haja ya wataalamu kuanza kujipanga kuchukua hatua za utekelezaji makubaliano, ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau upande sekta ya mawasiliano inakoelekea na kuchangamkia fursa zinazotokana na mapinduzi hayo ya mawasiliano duniani.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Dk. Jabiri Bakari, anathibitisha wataalamu kutoka taasisi yake wamejiandaa kuendana na mageuzi hayo ya kimahitaji, kutetea maslahi ya taifa kitaalamu, kuhakikisha nchi inaendelea sambamba na makubaliano yaliyofikiwa mkutanoni.

Kuhusu matokeo ya mkutano huo, anataja Tanzania imeongezewa masafa mapya yatakayowezesha huduma ya intaneti ya kasi (5G), ambayo ni muhimu katika kuchochea uchumi wa kidijitali.

Anataja hiyo ni zao la nafasi ya sekta ya mawasiliano ikiwa ni nyenzo wezeshi inayotoa ufanisi katika sekta nyingine, kama vile fedha, utalii, kilimo, afya, elimu, utangazaji, miundombinu, usafirishaji na maeneo mengine mengi.

Vile vile mkutano umeiwezesha Tanzania kupata ongezeko la masafa mapya yatakayotumika katika kuboresha usalama wa mawasiliano ya angani na majini (aeronautical and maritime communications).

Dk. Jabiri anataja ni masafa yatakayoongeza ufanisi katika mawasiliano ya ndege, usalama wa anga, maboresho ya kuongoza safari za majini na usalama wake, ikiwa ni pamoja na utabiri wa hali ya hewa.

Anafafanua kuwa, ni mkutano uliokuwa na manufaa makubwa kwa kuridhia teknolojia mpya kuanza kutumika, vifaa maalumu vya mawasiliano vitawekwa angani kuanzia kilometa 20 hadi 50 kutoka usawa wa Bahari, vitakavyofanya kazi ile ya minara ya mawasiliano ya simu.

Dk. Jabiri anasema, ni hatua inayowezesha zilizokuwa hazipati huduma ya mawasiliano vijijini, kufikiwa na mawasiliano ya simu na intaneti ya kasi katika ubora na kupaongezea ufanisi.

Hapo, mtaalamu huyo anasisitiza kwamba, eneo lingine ambalo la manufaa nchini ni kulinda matumizi ya televisheni za kidijitali kwenye bendi ya UHF ambayo ni masafa yanayohusika na utoaji huduma za utangazaji kupitia mitambo iliyosimikwa aridhini, yaani DTT.

Katika hilo anamaanisha kuwa uwekezaji kwenye miundombinu ardhini, utaendelea kulindwa na Watanzania watakaopendelea kupata huduma hiyo ya utangazaji, ili a kuwasiliana na kujiletea maendeleo.

Ni mkutano uliotoa mwelekeo wa maeneo mapya ya utafiti ambayo nchi wanachama wa Shirika la Mawasiliano Duniani, zinaweza kufanya tafiti ili kufanikisha maendeleo ya sekta ya mawasiliano.

Maeneo hayo, ni pamoja na tafiti zinazofanyika kwa kutumia satelaiti, ambazo zina uwezo wa kusafirisha takwimu za utafiti kwa haraka kupitia vituo vya utafiti.

Mchakato wa mapendekezo ya upangaji masafa, yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu ulioanza tangu mwaka 2020, kupitia Kamati ya Maandalizi ya Kitaifa, inayoundwa na orodha ya wadau maalum.

Hao wanatajwa kuwa: Kamati inayoundwa na wajumbe kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Miundombinu Zanzibar (MoIC); na Wizara ya Ulinzi.

Wengine ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Watoa Huduma za Mawasiliano (MNOs), Ofisi ya Rais (PO), Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Chuo Kikuu cha Dar- Es- Salaam (UDSM), Taasisi ya Teknolojia ya Dar Es- Salaam (DIT).

Pia, kuna Klabu ya Redio ya Armature Tanzania (TARC) na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Tanzania ikiwa Mwenyekiti wa Maandalizi ya WRC-23 kwa nchi za Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

# JWTZ yapeleka askari 300 kulinda amani Afrika ya Kati

**Na Mwandishi Wetu**

KIKUNDI cha maofisa na askari zaidi ya 300 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kimewasili eneo la Bangui, Jamuhuri ya Afrika ya Kati kwa ajili ya kulinda amani.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na JWTZ jana, kikosi hicho cha saba kitakachokuwa chini ya Luteni Kanali Joseph Mshilu, kinatarajiwa kutoa huduma nchini humo kulinda amani kwa muda wa mwaka mmoja na kitafanya kazi chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa, yaani (MINUSCA).

Kikosi hicho kimepokea majukumu yake kutoka kikosi cha sita kilichomaliza muda wake na kurejea nyumbani.

"Kikosi hiki kinatarajia kuendelea kuimarisha hali ya usalama magharibi mwa taifa hilo lililokumbwa na machafuko ya ndani. Miaka michache iliyopita makundi hasimu yenye misimamo mikali ya kidini ya Anti Baraka na Sereka yalihitilafiana na kusababisha machafuko," ilifafanua taarifa hiyo.

Kamanda wa Kikosi hicho, Luteni Kanali Joseph Mushilu, alisema, "Tanzania imejipanga kuimarisha hali ya usalama na kuendeleza yote yaliyofanywa na watangulizi wetu pia kulinda misafara ya huduma za kijamii kuhakikisha inafika salama na tunaishukuru Serikali ya Tanzania kutuwezesha kwa vifaa na mafunzo ambayo yametuweka tayari kutekeleza jukumu letu.

"Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa, imekuwa inashiriki ulinzi wa amani sehemu mbalimbali duniani ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Lebanon, Msumbiji, Sudan na maeneo mengine kwa kuchangia askari na waangalizi wa kimataifa," ilielezwa katika taarifa hiyo.



# Ashtakiwa kutoa taarifa za uongo kituo cha polisi

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Mashtaka umedai mahakamani kuwa mfanyabiashara Pravinchandra Chavda mnamo Oktoba 7, 2019 alitoa taarifa za uongo kuhusiana na upotevu wa hati tano za viwanja katika Kituo Kikuu cha Polisi, Dar es Salaam kwa lengo la kujipatia hati za upotevu wa mali hizo wakati akijua si kweli.

Hayo yalidaiwa mahakamani huko jana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga wakati akimsomea hoja za awali mshtakiwa Chavda mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Aron Lyamuya wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Chavda anakabiliwa na mashtaka manne ambayo ni kutoa taarifa za uongo kwa mtumishi wa umma, kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu, kughushi na kuwasilisha nyaraka za kughushi kwa lengo la kujipatia mali kinyume cha sheria.

Wakili Grace alidai kuwa Januari 10, 2022, mshtakiwa, akiwa ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, alijipatia kiwanja namba 1814 kilichoko eneo la Msasani Peninsular, baada ya kuwasilisha kwa Msajili wa Hati nyaraka ya uhamisho wa kiwanja hicho, akijifanya Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uwekezaji ya Sole ambayo ni mmiliki wa kiwanja hicho wakati akijua si kweli.

Alidai kuwa Oktoba 7, 2019, katika kituo hicho cha polisi, mshtakiwa huyo alitoa taarifa za uongo kuhusiana na upotevu wa hati tano za viwanja kwa lengo la kujipatia hati za upotevu wa mali hizo wakati akijua si kweli.

Aliendelea kudai kuwa mshtakiwa, akiwa mkoani Dar es Salaam, akijua na kwa lengo la kudanganya, alighushi nyaraka inayoitwa maazimio ya bodi, akijaribu kuonesha kwamba nyaraka hiyo ni halisi na imetolewa na Mkurugenzi wa Point Investment Ltd wakati akijua si kweli.

Mwanga aliendelea kudai kuwa Januari 10, 2002, mshtakiwa akiwa ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, aliwasilisha nyaraka hiyo ya kughushi kwa Msajili wa Hati akionesha kiwanja namba 1814 kilichoko Msasani Peninsula aliuziwa.

"Kutokana na mazingira hayo, mshtakiwa alikamatwa na kupelekwa katika kituo cha polisi na kuhojiwa na baada ya hapo alipelekwa mahakamani na kufunguliwa kesi hiyo," alidai Wakili Grace.

Baada ya mshtakiwa kusomewa maelezo hayo, alikubali taarifa zake binafsi na kukana mashtaka yote manne yanayomkabili. Wakili Grace alidai watakuwa na mashahidi 12 pamoja na vielelezo mbalimbali zikiwamo nyaraka.

Hakimu Lyamuya aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 19, mwakani kwa ajili ya kutajwa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), akiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, akionesha Tuzo ya Heshima na Utambuzi wa Mchango wa NBC aliyokabidhiwa katika kufanikisha msimu wa 17 wa Tuzo za Rais za Wazalishaji Bora wa Viwanda (PMAYA), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Benki ya NBC ni mdhamini mkuu wa tuzo hizo za kila mwaka kwa mwaka wa pili mfululizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabasi kupewa wakala, chanzo ajali zisizoisha

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Madereva wa Masafa Marefu, Hassan Dede, ameeleza namna mawakala wa mabasi ya mafasa marefu wanavyochangia ajali za barabarani nchini.

Katika mazungumzo na waandishi wa habari jana kwenye mkutano mkuu wa nne wa mwaka wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TAMSTOA), Dede alisema madereva wengi wamekuwa wanaendesha kwa mwendokasi kwa shinikizo la mawakala hao wa mabasi ambao pia huhatarisha vibarua vyao.

Alisema madereva ambao hushindwa kutekeleza maelekezo ya mawakala ya kuendesha mabasi kwa mwendokasi, taarifa zao hupelekwa kwa wamiliki na kufukuzwa kazi.

"Dereva anaendesha basi, lakini anapewa maelekezo na wakala aliyekabidhiwa chombo na mmiliki, anamwambia dereva kwamba tunaomba uongeze mwendo, akipitwa na basi la nyuma, inatumwa taarifa ofisini kwamba huyu dereva hatembei na kama hatembei (haendeshi kwa kasi) anafukuzwa kazi.

"Kwahiyo, ili nisifukuzwe kazi inanilazimu nitembee mwendo ambao siyo wa kwangu na matokeo yake ndio hayo madhara makubwa kama haya ambayo tumekuwa tunashuhudia kila siku ya ajali zisizoisha," alisema.

Alisema changamoto nyingine wanayokutana nayo madereva hao ni kutokulipwa mishahara na kwamba licha ya serikali kuweka kiwango cha wao kulipwa, wapo baadhi ya wamiliki ambao wanashindwa kutekeleza hilo.

"Maslahi bado ni madogo, huwezi kuwa dereva ambaye unaendesha chombo cha Sh. milioni 600 halafu unalipwa mshahara wa Sh. 300,000. Maana yake kwa siku ninatumia Sh.10,000, haitoshi.

"Pamoja na Rais Samia Suhulu Hassan kupandisha kiwango cha chini cha mishahara kutoka Sh. 150,000 mpaka Sh. 330,000 kwa dereva, lakini kuna baadhi ya wamiliki hawataki kulipa hata hicho kiasi, madereva wengine wanalipwa hadi Sh. 100,000 na wengine hawalipi kabisa mishahara.

"Kwahiyo, tusitegemee kwamba nchi hii itakuwa salama au kumaliza ajali za barabarani kutokana na changamoto hizi," alisema Dede.

Mwenyekiti wa TAMSTOA, Chuki Shaban, alisema kwa sasa kwenye chama chao wamemaliza malalamiko yote yaliyokuwa yanajitokeza hususani katika ulipaji mishahara kwa madereva na kuvitaka vyama vingine vya wasafirishaji kuiga mfano wao na kuwathamini madereva wao.

"Sekta hii ya usafirishaji, ina mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi na tunapozungumzia mchango huo, miongoni mwa wanaochangia ni pamoja na hawa madereva. Kwa hiyo, kuwathamini ni jambo la msingi," alisema Shaban.

Aliwataka madereva kujiunga kwenye vyama ili changamoto zao zizungumzwe na kutatuliwa kupitia vyama vyao.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wiki iliyopita, kwa kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka huu, ajali zilizotokea ni 1,641 na kati yake, 1,057 zilisababisha vifo huku 451 zikisababisha majeruhi wakati ajali 135 zilisababisha uharibifu wa vyombo vya moto.

Ajali hizo zilisababisha vifo kwa watu 1,550 na kati ya hivyo, vifo vya wanaume vilikuwa 1,189, na wanawake 361.

Majeruhi katika kipindi hicho, walikuwa 2,562 na kati ya hao, wanaume walikuwa 1,721 na wanawake ni 841.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# RC Serukamba kabili uchafu huu kimkoa, moshi unafuka

**KAULI** ya kwanza, kuna hoja yenye sifa zote za kuitwa mjasiri, mzalendo na mzazi, pale Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda alipoanika mambo machafu yanayofanyika dhidi ya wanafunzi wilayani mwake, hata kuwakwamisha safari zao za masomo.

Mwenyekiti huyo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Iramba, alianika mikasa ya mimba, mabinti kuolewa na kufanywa unajisi, hali inayoathiri hata kunashuhudiwa utoro mkubwa miongoni mwa wanafunzi walioko shule za msingi na sekondari.

Ni hoja alizoanika kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) wa Singida siku chache zilizopita. Maumivu zaidi ni kwamba wanaofanya hayo ni wanafunzi wanaoonekana kubobea katika hayo, wakiwa na fedha za kuwahonga wanaotendwa hayo.

Hapo ndipo Nipashe inaweka nukta katika maelezo tajwa na kuhoji kuna nini tena na yule anayetenda, hali kadhalika anayetendwa, wanapata wapi ujuzi huo mchafu, pia nguvu za kuwezeshana?

Inaumiza kusikia wanafika hatua kuwa na stadi za kutumia saikolojia ya watu wazima kuhonga, ikizua swali lingine, fedha za matumizi hayo wanazipata wapi?

Tayari kuna dosari kitaifa. Sura ya kwanza, ndani ya kundi hilo la watoto wanaoandaliwa kubeba dhamana za kusimamia taifa, wanakinzana na yote yanayopingwa na nchi kimaadili na hata kisheria, ikiwamo inayounda Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Jasiri DC Mwenda, Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama Iramba akatamka picha ya kwanza ya udadisi wake kiusalama alikofanya utafiti, akitumia kauli:

"Tuna hisia hawa watoto wanaofanya hivi vitendo, kuna watu wako nyuma yao, kwa sababu wana fedha za kuwahonga wenzao, japo wazazi ni maskini. Wapo wengine wanatembea na mafuta maalum ya kufanya shughuli hiyo. Tunajiuliza, vitu hivi wanatoa wapi?"

Kwa maoni yetu Nipashe, kasoro hii ya kijamii inapaswa rasmi kuwa ajenda ya kimkoa huku mamlaka za kitaifa zikianika kurunzi kufuatilia hatua za marekebisho.

Maadili yanaporomoka na elimu pia inaporomoshwa. Je, mahali pa kushikilia patakuwa wapi? Moja kwa moja, Mkuu wa Mkoa, Peter Serukamba, una wajibu wote kuingiza katika orodha ya ajenda zako kuu katika usalama wa mkoa na kuingia vitani na timu yako, wakiwamo wakuu wa wilaya.

Penye wakala wa kuvusha na kupokea watoto hao, kwenda kufanya kazi za ndani, wakiacha shule au kwenda kuolewa au kufanya kazi Dar es Salaam na kwingineko, nayo iwe ajenda. Ndio maana ya ulinzi na usalama, dhamana uliyokabidhiwa kimkoa.

Ni maumivu yanayofika huko, shule ikiwa ndio mtetezi mkuu wa maisha ya mtoto, afya na usalama ikimtetea katika safari hiyo. Hapana shaka picha pana ya kilio cha Mkuu wa Wilaya ya Iramba dhidi ya utoro mimba na unajisi inapaswa kuvaliwa miwani kimkoa, hata ukaingia 'vitani'.

Tayari sumu inashuhudiwa kuanzia anavyoainisha Mwenda, kwamba mwaka jana kuna shule ikawa na wanafunzi wawili pekee, ndio waliofaulu kati ya 23 waliofanya mtihani.

Baada ya uchunguzi kukabainika shule hiyo iitwayo, Mwamapuri, inaelemewa na changamoto ya wanafunzi kuolewa kabla ya kuhitimu elimu ya msingi.


Lingine baya kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya - Mwenda, kinara wa kuwafanyia watoto unajisi akaonesha alivyozama katika tabia hiyo. Mtuhumiwa huyo alipopewa dhamana kwa shtaka la unajisi, akarejea tena kwenye wilaya mbili nyingine kutenda kama hayo akiwa kwenye dhamana nyingine aliko.

Hapo napo inatoa ishara ambayo kunapofuka moshi, kuna moto, kwamba ndani ya wilaya hizo ambazo mtuhumiwa anatajwa kuonekana na dhambi kisheria nazo ni shida, kwa maana nako si salama.

Kuwapo wasichana wa Iramba wanaovushwa kwa wingi kwenda mkoani Dar es Salaam, kufanya kazi za ndani ni dosari katika ulinzi na usalama wa watoto.

Katika sura ya kawaida inazalisha ishara gani katika safari ya maendeleo ya mkoa Singida? Wanazuoni wameshatafsiri dhana maendeleo ni hali ya maboresho katika idadi na viwango vya yale wanayopaswa kupata jamii husika. Uongozi wa mkoa una kazi ya kufanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Konda na dereva washiriki wizi huu

**KUELEKEA** sikukuu za mwisho wa mwaka za Noeli na Mwaka Mpya ni wakati wa kutafakari na kujali zaidi usalama wa kila mwanafamilia na jamii.

La muhimu na la kwanza ni ulinzi wa watoto wasidhuriwe, ni vyema wazazi na walinzi wakalikumbuka hili.

Aidha, kuna suala la watu wazima kuporwa na vibaka gizani hasa kwenye mitaa yenye giza au msongamano.

Lakini kuvamiwa nyumbani na kuibiwa mali kuanzia mifugo mfano ng'ombe, mbuzi na wanyama wengine wadogo wakiwamo kuku na bata pia.

Aidha, barabarani si salama wezi wa magari, pikipiki na mizigo wakati wa safari ni mambo yanayohitaji kukumbushana.

Leo nizungumzie suala la makonda wa daladala mijini ambao wanashutumiwa kushirikiana na vibaka wanaopanda kwenye magari yao.

Ni kwa sababu wanawafumbia macho wezi hao, kuna madai kuwa wanawaweka wasafiri kwenye wakati mgumu pale wanapo waruhusu wezi na wadokozi, wapande kwenye daladala na kuiba.

Abiria hasa wa majiji makubwa na miji midogo wanaamini kuwa wanawafahamu vibaka na wezi hao kwa kuwa kila leo wanakutana nao na wanazielewa sehemu wanapopandia na kushukia kwenye basi.

Nyakati za msongamano ndani ya basi wapo vibaka au wapigadebe wanaopanda daladala sehemu zisizo rasmi na kuomba kushushwa maeneo yenye giza ili wasifahamike, katika hili makondakta watajiteteaje?

Ndiyo maana abiria wanaamini kuwa makonda wanashirikiana na vibaka kuwaibia watu ndani ya daladala.

Inashangaza mwaka 2023 miji na majiji yanajaa kelele za wapiga debe kuita abiria. Wengi wanajiuliza hivi watu hawajui kusoma magari na kupanda mpaka waambiwe au kutangaziwa?

Vituo vimejaa watu wengi wanaohudumia abiria, inafika kipindi hushindwa kuwatofautisha makondakta, wapiga debe na wezi au vibaka, hivyo makonda na madereva msaidie kulinda usalama si wakati huu wa siku kuu lakini muda wote.

Jambo la ajabu zaidi hata katika vituo vikubwa vijana wanaochipukia huacha shule na kujikita kwenye kuita abiria wa mikoani.

Ni usumbufu kila mahali abiria wakiingia vituoni iwe Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma wanakutana na makaribisho kuulizwa unakwenda mkoa gani?

Kulakiwa huko ni kero na wengi wanaibiwa mali zao baada ya kuzongwa na kuvutwa huku na kule kisa eti wanapelekwa kufikia mabasi ya mikoani wanayoyaendea.

Ni usumbufu zaidi kwa wageni ambao husumbuliwa muda wote kwa sababu hawaelewi na hawana msaada mbali na huo wa wapigadebe wa safari za mikoani.

Vijana waachane na fikra mgando, waondoke kwenye mtazamo hasi fursa na kazi ndogo ndogo zipo nyingi kuna biashara, kilimo na ufugaji, sanaa, muziki na kandanda kulikoni kuhatarisha maisha yenu kwa kung'ang'ania kazi zisizotumia nguvu wala maarifa.

Inakuwaje uendelee kuamini kuwa kupigadebe kutafanikisha kujenga maisha yako na ya kizazi kilicho imara cha sasa na kijacho kwani , watoto huiga tabia kwa wakubwa na wazazi au walezi wao ni vyema kuamua kutoka gizani ili kuandaa maisha bora yanayojengwa na msingi imara wa kufanyakazi.

Ni wazi kuwa kazi ya kupiga debe ni kama uzururaji wanaojihusisha na kazi hiyo huonekana kama wezi au vibaka au watumia dawa za kulevya au wahalifu.

Rai kwa makonda wa daladala wasiruhusu au kushirikiana na vibaka kwa kuwaruhusu kupanda kwenye magari kwani wanafanandishwa nao kwa imani kuwa wamepanga mchongo ili kuibia abiria,

Wito kwa serekali itoe elimu kwenye makundi ya vijana wanaojiingiza kwenye kazi hiyo ya kupiga debe na kuwapa fikra mbadala ili kuwabadili tabia.

Wapigadebe wadhibitiwe na mambo hayo yakatazwe kisheria ili mipango ya kuelekea kwenye mfumo wa kielektroniki kwenye usafiri ifanikiwe.

Walimu shuleni watoe mafunzo ya athari za kukwapua, wizi kwenye jumuiya na ndani ya jamii lakini pia wakiwapa wanafunza mbinu za kuwa shupavu na kujitegemea.

Wazazi , walezi na walimu wakiandaa misingi iliyo imara kwa watoto au vijana kuna uwezekano wa kudhibiti, utapeli, wizi na ulaghai kwa kizazi hiki na kijacho.

Vijana watamani kazi zenye heshima badala ya kupigadebe, kuuza bidhaa duni kama toi, kujazana sokoni na kung'ang'ania wateja kuwabebea mizigo na kukimbiza abiria wanaoshuka kwenye mabasi mijini wakiwauliza unaelekea mkoa upi?

## TANROADS yarejesha mawasiliano Tabora

**Na Frank Monyo**

WAKALA wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Tabora umerejesha mawasiliano ya barabara ya Bukumbi- Kahama ambayo ilikatika kutokana na gari la mizigo kuzidisha uzito na kupasua kalvati ambalo lilisombwa na maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Juzi, Meneja wa TANROADS Mkoa wa Tabora, Raphael Mlimaji alisema eneo la barabara lililokatika ni kati ya Kijiji cha Muhulidede, Kata ya Ishihimulwa, Wilaya ya Uyui, umbali wa kilomita 108 toka mjini Tabora na Kijiji cha Busule, Kata ya Chona, Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga; Km nne kutoka mjini Kahama.

"Mnamo Desemba 14, mwaka huu, majira ya saa tisa usiku, gari la mizigo aina ya fuso lililokuwa limebeba shehena ya karanga lilipita katika barabara hiyo inayounganisha Mkoa wa Tabora na Shinyanga kupitia Wilaya za Uyui na Kahama,

"Kutokana na kuzidisha uzito na siku hiyo mvua kubwa ilinyesha eneo hilo, gari lilipasua kalvati ambazo zilijengwa zamani kwenye barabara hiyo ambayo awali ilikuwa ni ya halmashauri na baadaye kuletwa TANROADS ili ifunguliwe iwe inapitika wakati wote," alisema.

Mlimaji alisema kufuatia athari hiyo, TANROADS iliamua kukata maeneo manne tofauti na kupanga mawe, ili kuwezesha maji yatakayokuwa yameongezeka kupita chini wakati vyombo vya moto na watu wakipita juu ya barabara pasi na kusitisha shughuli za usafiri na usafirishaji.

Alisema barabara hiyo inapitisha shehena nyingi zinazotoka mikoa mbambali ikiwamo Katavi, Mbeya na maeneo ya jirani kutokana na kuwapo maghala mengi ya chakula Kahama ambayo pia yanahudumia nchi za Burundi, Rwanda na Kenya.

Alisema kutokana na hatua zilizochukuliwa na serikali, kwa sasa barabara hiyo inapitika.

# Mikopo 'kausha damu' yaishtua BoT

**Na Christina Mwakangale**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imezindua mtaala mpya wa elimu ya fedha kwa wakufunzi kwa lengo la kukuza uelewa kwa umma katika utafutaji, utumiaji, uwekaji akiba na dhamana, ukopaji na utawala.

Mtaala huo uliowalenga wasimamizi wa sekta ya fedha, kampuni, taasisi za umma na binafsi, asasi za kiraia, vilabu na mashirikia yasiyo ya kiserikali, utaanza kutumika mapema mwakani.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, akizindua mtaala huo juzi jijini Dar es Salaam, alisema programu hiyo kwa makundi hayo, ina lengo la kuongeza uelewa kuhusu fedha nchini.

Alisema elimu ni duni miongoni mwa Watanzania katika masuala ya fedha, ikiwamo wasomi katika kada tofauti, akisema baadhi yao huwa na dhana kwamba hawahusiki na uelewa huo.

"Athari ya elimu duni huchangia ongezeko la umaskini.

Ninaagiza ndani ya miezi miwili mtaala huu utafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili na upatikane katika tovuti ya BoT. Pia uwe katika mfumo wa sauti na video kwa sababu wengine hawapendi kusoma, bali kusikiliza na kutazama.

"Elimu hii iwe na ubunifu, endelevu na shirikishi na itumie teknolojia yaani TEHAMA, kwa sababu ndiko dunia iliko, mtaala huu upime matokeo ya mafanikio kila baada ya muda fulani," alisema Tutuba.

Awali Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'I Issa, akizungumza katika mjadala kuhusu matarajio ya mtaala huo, alisema elimu hiyo itausaidia umma kufahamu namna ya kuzitawala fedha.

Alisema kwa asilimia 54 ya wanawake nchini waliojikita katika ujasiriamali wa kati na mdogo, hawana elimu kuhusu fedha, jambo linalowasababisha kuingia kwenye mikopo yenye riba kubwa.

"Mikopo ya 'kausha damu' inawakumba hasa wanawake na vijana. Watu wafundishwe kuzitawala fedha, si fedha ziwatawale wao," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Asasi Zinazotoa Huduma Ndogo za Kifedha (TAMFI), Winnie Terry, alisema malengo ya taasisi za kifedha awali yalikuwa kuinua jamii, lakini sasa mahitaji yanavyoongezeka, kuna ongezeko la changamoto.

"Microfinance (huduma ndogo za kifedha) ililenga watu wa chini ambao hawana dhamana. Leseni na elimu yao ya fedha ni ndogo kutokana na benki rasmi kuwa na vigezo vigumu kwa kundi hilo. Sasa taasisi za zimeongezeka.

"Changamoto inakuja wao wanatangaza tu wanatoa mikopo, ila baadhi ya taasisi inachukulia udhaifu wa kundi hili na kutotoa elimu, utakuta taasisi imejaa friji, televisheni, redio kwa sababu mkopaji kashindwa kulipa," alisema Terry.



Mkazi wa Mtaa wa Iganana, Kata ya Nkende wilayani Tarime, Mwita Juma (kulia), akielezea kero zake kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (wa pili kushoto waliokaa), katika mkutano wa kliniki ya ardhi uliofanyika ofisi ya zamani ya Halmashauri ya Mji wa Tarime juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maabara Mkemia Mkuu yapongezwa kuchunguza sampuli kwa muda mfupi

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

MRAKIBU Mwandamizi wa Polisi, Adam Salim Amiri, ameipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) kwa kuchunguza sampuli za makosa ya jinai kwa muda mfupi na kukamilisha upelelezi haraka na mashauri kusikilizwa mahakamani kwa wakati.

Alitoa pongezi hizo jana wakati Mkuu huyo wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Mtwara alipofungua Mafunzo ya Usimamizi wa Sampuli za Makosa ya Jinai yaliyofanyika jana wilayani Masasi, Mtwara.

Mafunzo hayo yalijumuisha maofisa wa Jeshi la Polisi kutoka mikoa ya Lindi na Mtwara, madaktari na wataalamu wa maabara wanaohusika na mnyororo wa sampuli za makosa ya jinai.

"Ninapenda kuipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika uchunguzi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali za makosa ya jinai na kusaidia kukamilisha upelelezi kwa wakati na mashauri kusikilizwa mahakamani kwa wakati na hivyo kuchangia upatikanaji haki kwa wakati," alisema Amiri.


Alisisitiza kuwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau ambao wanahusika katika mnyororo mzima wa uchukuaji sampuli au vielelezo na kuviwasilisha ofisi ya mkemia kwa uchunguzi wa kimaabara ni muhimu, kwa vile upatikanaji matokeo sahihi ya uchunguzi wa vielelezo hivyo, huchangiwa kwa kiasi kikubwa na ufanisi wa hatua za awali za uchukuaji vielelezo hivyo, ufungashaji na usafirishaji.

Amiri alisisitiza umuhimu wa uchunguzi wa kisayansi katika ulimwengu wa utandawazi kuwa ndio msingi mkubwa wa kujenga kesi mahakamani.

Kaimu Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kusini, Hosea Hosea, alisema mafunzo hayo yakitumiwa kwa usahihi, yatasaidia ukusanyaji wa sampuli, ufungashaji sampuli na usafirishaji sampuli ulio sahihi ambao utasaidia mamlaka kufanya uchunguzi na kupata majibu sahihi ambayo mwisho wa siku yatasaidia upelelezi na utoaji haki.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



# Serikali yatoa ufafanuzi kituo kinachodaiwa kukosa vitanda

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amekanusha taarifa inayosambaa mitandaoni ikidai kuwa katika Kituo cha Afya Buzuruga, wilayani Ilemela mkoani Mwanza, wajawazito wanapeana zamu kujifungua katika kitanda kimoja huku wengine wakijifungulia sakafuni.

Ametoa ufafanuzi huo kutokana na taarifa iliyosambazwa juzi katika mtandao wa kijamii wa X, ukimtaka afuatilie kituo hicho cha afya kutokana na madai kwamba wajawazito wanajifungulia sakafuni.

Baadaye katika mtandao wake wa X, Waziri Ummy alitoa ufafanuzi kuhusu taarifa hiyo, akieleza kuwa huduma katika kituo hicho zimeboreshwa na zinaendelea kuboreshwa.

"Hivi sasa asilimia 81 ya wajawazito nchini wanajifungulia katika vituo vya kutoa huduma za afya kulinganisha na asilimia 63 kwa mwaka 2016 na vifo vya wajawazito vimepungua kutoa 556 kwa kila vizazi hai 100,000 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000," alisema.

Alikiri sekta ya afya inabadilika mara kwa mara, hivyo kila siku zinaibuka changamoto mpya na zote haziwezi kuisha kwa siku moja wala kipindi kimoja, hivyo zinachukuliwa hatua mahsusi kuzitatua kwa haraka huku huduma za mama na mtoto zikipewa kipaumbele zaidi.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachuzibwa, aliiambia Nipashe juzi kuwa taarifa hiyo si ya mwaka huu kwa kuwa kituo hicho kinavyo vitanda sita na viliongezwa baada ya ongezeko la wahitaji kutoka vitanda vitatu vilivyokuwapo awali.

"Hiyo taarifa tumeipata lakini tayari tumetoa taarifa ya kuujibu ujumbe huo uliosambazwa kupitia mitandao ya kijamii, ukifuatilia vizuri utauona," alisema Dk. Rutachunzibwa.

Katika taarifa ya ufafanuzi iliyotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Wakili Kiomoni Kibamba, ilibainisha kuwa picha hiyo ilipigwa Septemba 2022 na si ya mwaka huu.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa serikali baada ya kuona kituo hicho kimekuwa na ongezeko la kinamama wanaojifungua, iliongeza vitanda vingine vya kujifungulia kutoka vitatu hadi sita, hivyo kituo hicho kinavyo vitanda, tofauti na ujumbe unaosambaa. Vilevile, taarifa hiyo ilifafanua kuwa kituoni huko kumejengwa jengo la mama na mtoto lenye uwezo wa kulaza kinamama 42, likigharimu Sh. milioni 200 (fedha za ndani).

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa lengo la ujenzi huo ni kuondoa adha ya kinamama kulala zaidi ya mmoja kwenye kitanda kimoja na jengo hilo tayari limeanza kutumika baada ya kuzinduliwa na Mwenge wa Uhuru, mbali na chumba kilichowekwa mtandaoni.

"Kwa maelezo hayo, halmashauri inapenda kuuhakikishia umma kuwa katika kituo hicho hakuna kinamama wanaojifungulia chini kama taarifa ya mtandao inavyoonesha," ilielezwa katika taarifa hiyo.



Mbunge wa Jimbo la Ilala, Mussa Azzan Zungu, akizungumza katika mkutano wa semina ya mafunzo ya Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Tanzania Kiuchumi ulioandaliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Taasisi dini yajipanga kutekeleza agizo la Rais kupokea wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Sunni Muslim Jamaat ya jijini Dar es Salaam imesema iko tayari kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kupokea na kuandikisha watoto wanaotarajiwa kujiunga na darasa la kwanza mwakani.

Katibu Mtendaji wa jumuiya hiyo, Muhammad Waseem, alisema jana jijini kuwa wamepokea agizo hilo la Rais Samia na wako tayari kushirikiana naye katika kupokea watoto wengi kujiunga na shule zao ili kuondoa tatizo la ukosefu wa nafasi katika shule za serikali.

Waseem alisema jumuiya hiyo inayo shule katika Mtaa wa Mindu Upanga jijini ambayo kuanzia mwakani itaandikisha wanafunzi 500 mpaka 600, idadi ambayo itasaidia kupunguza tatizo la wanafunzi kukosa nafasi katika shule za serikali.

Waseem alisema mbali na kuwaandikisha watoto kujiunga na shule zao, pia watapata fursa nyingine ya kupatiwa bima ya afya itakayotolewa na jumuiya hiyo kama msaada kwa watoto hao watakaojiunga na shule zao ili kuboresha afya zao pamoja na kupata elimu bora.

"Jumuiya imejipanga vizuri katika kusaidia serikali ya Rais Samia ambayo imeonesha kuthamini na kujali taasisi na jumuiya za kidini nchini kuwa zina mchango mkubwa katika kusaidia maendeleo ya elimu, afya na uchumi," alisema.

Waseem alisema shule za jumuiya hizo zinatoa elimu bora bila ya kubagua dini, kabila, rangi wala madhehebu na wanapokea watoto wote kwa ajili ya kupata elimu.

Katibu mtendaji huyo alisema mbali na kutoa huduma ya bima ya afya, pia wanatoa huduma za usafiri kwa wanafunzi wote wanaosoma katika shule hizo pamoja na huduma ya chakula shuleni.

Mmoja wa wazazi jijini Dar es Salaam, Rahma Hamza, alisema amefurahishwa na juhudi za Jumuiya ya Sunni Muslim Jamaat kuanzisha shule ya awali na msingi yenye lengo la kutoa elimu, huku wanafunzi wakikatiwa bima ya afya.

Alisema shule nyingi za msingi, hazina utaratibu wa kuwapatia bima ya afya wanafunzi wao, hivyo jumuiya ni mfano wa kuigwa.

Rais Samia mwishoni mwa wiki wakati wa awamu ya 17 ya Tuzo za Rais kwa Wazalishaji Bora wa Viwanda nchini, aliagiza wanafunzi wote wadahiliwe mwakani.

Aliziomba taasisi na jumuiya zote za kidini nchini kujitolea katika shule zao kuandikisha wanafunzi watakaojiunga darasa la kwanza mwakani ili kuondoa tatizo la upungufu wa madarasa katika shule za serikali.

Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, anasema katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', kuwa "ombi la Rais ni agizo".

## Mawakala wapewa angalizo mfumo wa mbolea ya ruzuku

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA) imesema itachukuliwa hatua kali dhidi ya mawakala wa usambazaji mbolea ya ruzuku watakaobainika kuchezea mfumo wa ruzuku.

Kaimu Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Allan Mariki, alitangaza hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari mjini Morogoro baada ya ufunguzi wa mafunzo kwa wakaguzi tarajali wa mbolea ambao ni maofisa kilimo kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Maofisa hao wanatoka mikoa ya Shinyanga, Morogoro, Kilimanjaro, Simiyu na Mtwara. Wanapatiwa mafunzo kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye ukaguzi wa mbolea nchini.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TFRA alisema kutokana na mawakala hao kufanya vitendo vya udanganyifu kwa kuchezea mfumo huo, sasa wameongeza timu ya wakaguzi.

Alisema timu hiyo ya wakaguzi kuanzia sasa itakuwa inapita moja kwa moja kwenye maduka ya mawakala, mashamba ya wakulima na maghala yao kuhakikisha mbolea inayotumika ina ubora.

"Tunaonya mawakala wa kusambaza mbolea ya ruzuku kuwa hivi sasa tumejipanga kikamilifu, waache kuchezea mfumo wetu na kufanya udanganyifu. Kuanzia sasa tutakayembaini kuchezea huo mfumo, tutamchukulia hatua kali sana na hatutakuwa na huruma kwa yeyote," alionya.

Alisema TFRA imeweka lengo la kuwa na wakaguzi wawili kwa kila halmashauri ili kuimarisha ufanisi katika udhibiti wa mbolea nchini.

Mariki pia alitoa rai kwa wenye maduka ya pembejeo, kuepukana na udanganyifu wa kusambaza mbolea zilizochanganywa na malighafi nyingine kwa kuwa watakapobainika, watachukuliwa hatua za sheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Kuhusu mafunzo ya maofisa hao, alisema wakimaliza mafunzo hayo watapewa majukumu ya kuwa wakaguzi wa mbolea kwa mujibu wa vifungu 33 na 34 vya Sheria ya Mbolea. Pia watakuwa na mamlaka ya kukagua malori, maduka, meli na majahazi.

Alitaja maeneo mengine ni kwenye ndege, posta, bohari ya mbolea, stoo za mbolea, garimoshi na mahala patakapohitajika.

Katika kutekeleza wajibu huo wa udhibiti wa mbolea, alisema mamlaka imekuwa inafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maghala ya kuhifadhi mbolea.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Morogoro, Dk. Rozalia Rwegasira, alisema Tanzania katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita imekuwa inatumia tani 300,000 hadi 600,000 za mbolea mbalimbali kwa mwaka. Zaidi ya asilimia 90 ya mbolea hizo huagizwa kutoka nje ya nchini.

Alisema mbolea ni mojawapo ya pembejeo muhimu kati ya pembejeo tatu zinazohitajika katika kuongezea tija kwenye uzalishaji wa mazao, hivyo ili kuhakikisha mkulima anapata mbolea bora, udhibiti mbolea unahitajika.



## TRA yajivunia mafanikio ya ETS kwa miaka mitano

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MFUMO wa matumizi ya stempu za kielektroniki (ETS), unaotumiwa na Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Manyara (TRA), mpaka sasa umefanikiwa kuwasajili walipa kodi pekee 620 kwa miaka mitano.

Stempu hizo zinatajwa kupunguza wimbi la uingizaji wa bidhaa bandia za vinywaji vikali, ikiwamo pombe na mvinyo.

Akizungumzia jana mafanikio hayo katika Mji wa Babati, Meneja Mradi wa ETS Makao Makuu, Abyud Twelve, alisema mfumo huo ulioanzishwa Januari 15, mwaka 2019, umesaidia kuongeza kiwango cha uzalishaji wa bidhaa za vinywaji vikali.

"Lengo la mfumo huu ni kudhibiti, kusimamia na kuongeza udhibiti wa stempu ili mfumo uwe na tija kwa wazalishaji na wasafirishaji wa nje," alisema Twelve.

Aidha, alisema mfumo huo umewasaidia kupunguza watu wanaouza bidhaa za magendo, na kwamba wanaobainika wana makosa huburuzwa kortini.

Alisema sheria inawaelekeza wazalishaji wa viwanda kubandika stempu kwenye bidhaa zao, na wauzaji nao kuwa na bidhaa zenye stempu na kutoa stakabadhi za kielektroniki (EfD) kwa wateja wao.

Kutokana na sheria ya udhibiti wa mapato, mfanyabiashara ambaye anakiuka sheria hiyo, faini yake haipungui Sh. milioni tano na haizidi Sh. milioni 50, au kifungo cha miaka mitatu jela.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Twiga General Traders Limited, Richard Ngalewa, ambao ni wauzaji wa vinywaji vikali, alisema mfumo wa ETS ni mzuri na umeletwa kwa wakati.

**Aidha, alisema mfumo huo umewasaidia kupunguza watu wanaouza bidhaa za magendo, na kwamba wanaobainika wana makosa huburuzwa kortini.**

# Tusonge kuja na mwarobaini wa mabadiliko ya tabianchi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHIRIKA la Maendeleo ya Jamii la Tusonge limetangaza kuja na mpango mahsusi wa miaka mitano wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi yanayotajwa kuchochea ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Akizungumza katika Mkutano wa 12 wa shirika hilo, Mkurugenzi wake, Aginatha Rutazaa, alisema mpango huo ni moja kati ya mambo watakayoyaongeza katika kipindi cha mwaka ujao.

Alisema athari hizo zinawatesa wanawake wanajikuta wakiingia katika ukatili kutokana na mahitaji hayo kukosekana ikiwamo maji ya kuhudumia familia na kuni za kupikia.

Alisema mpango huo pia unalenga kuwapunguzia wakulima changamoto ya uzalishaji kutokana na vikwazo vya mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa taifa.

Alisema lengo ni kuunga mkono serikali katika utekelezaji wa kilimo rafiki kwa mazingira, ambacho kinaweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kama vile umwagiliaji.

"Mabadiliko haya yana athari kubwa za kukosekana kwa mvua na wakulima wanakosa mazao ya chakula. Kuna ukame na kukosekana kwa maji, waathirika wakubwa ni wanawake, wasichana na watoto," alisema.

Kwa mujibu wa Rutazaa, eneo jingine linaloundiwa mkakati katika mpango huo mpya wa afya ya uzazi.

Alisema katika suala hilo wamejipanga kutoa elimu kwa wasichana rika balehe na kuwapa ujasiri wa kutumia uelewa na stadi, kufanya uamuzi sahihi kuhusu mwili wake na maisha yake.

"Hili tunaliangalia sana kwa wasichana wanaobalehe, ambao kwa kiasi kikubwa katika jamii zetu za kitanzania kule vijijini, hawazungumzi wazi wazi masuala yanayohusiana na afya ya uzazi na ngono salama.

Zaidi aliongeza, "Jambo hili limekuwa ni tatizo, kwa sababu jamii yetu na makuzi yetu, mara nyingi kuzungumza masuala ya ngono wazi wazi na watoto wetu, hasa wa kike ni ngumu. Ndio maana limekuwa linalochochea kuongezeka kwa ukatili wa kingono, hasa kwa kundi la wasichana balehe."




Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja (wa pili kulia), akipokea magodoro jana ikiwa ni sehemu ya msaada kwa waathirika wa mafuriko wilayani humo kutoka kwa Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Victus Valerian. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Haki ya wanawake, watoto kumiliki ardhi bado tatizo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

LICHA ya mradi wa majaribio ya utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya kifamilia nje ya vyombo vya Mahakama na Polisi (ADR), kupata matokeo chanya katika kesi za ndoa, mirathi na haki ya kumiliki ardhi kwa watoto wa kike bado changamoto.

Hali hiyo inatokana na vyombo vinavyofanya kazi hiyo, kukosa mamlaka au nguvu ya kisheria ya kutoa wito wa lazima kupatikana kwa haki hiyo.

Hayo yalisemwa jana na Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Muhusin Kirua, katika kikao kazi cha wadau wanaotekeleza mradi huo, Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Shirika la Legal Service Facility Tanzania (LSF).

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni kutoheshimu uamuzi au maridhiano yaliyofikiwa, baada ya kufanya maridhiano ya wenye kesi kubadili mawazo wanapofika hatua ya kusikilizwa.

"Watu wengi wana ile dhana ya kukengeuka, mnapofika mmekaa vikao vya utatuzi wa mgogoro wa kifamilia, hasa wazazi wawili wanapokuwa wametengana au kuachana mkaamua sasa tunafanya uamuzi, mteja anakengeuka anasema kwani mtanifanya nini," alifafanua.

Kiongozi wa kundi la wasaidizi wa kisheria, linalotekeleza mradi huo, Justine Lasway, alisema wanaridhishwa na mafanikio makubwa ya utatuzi wa migogoro kupitia njia hiyo.

Alisema moja ya mafanikio walioyapata kupitia ADR ni njia fupi ya utatuzi wa migogoro na kumaliza kabisa malumbano ya kifamilia hali inayochochea kuwapo na amani katika familia.

"Jamii imeipenda njia hii ya ADR na kuipokea vizuri kama mkombozi wa migogoro kwenye jamii nzima. Wanufaika wamepata haki zao bila gharama, na pia uelewa juu ya huduma hii umekuwa mpana," alisema.

Mratibu wa KWIECO/ADR, Lilian Mandari, lengo kuu la mradi huo ni kuchangia utatuzi wa migogoro ya kifamilia kwa kutumia njia mbadala ya utatuzi wa migogoro kwa ufanisi na kupunguza mashauri yanayoweza kutatuliwa kwenye jamii.

Alisema unalenga kuimarisha maarifa kwa watoa huduma za msaada wa kisheria, kwa kutumia njia mbadala ya utatuzi wa migogoro ya kifamilia, kuongeza uelewa wa jamii kuhusu sheria na kuimarisha mfumo wa kifamilia katika utatuzi wa migogoro kwa kuzingatiwa viwango vya sheria nchini.

Kwa mujibu wa Mandari, faida nyingine ya ADR ni kuokoa gharama, kwa sababu unapofungua shauri mahakamani, kuna gharama za ada unatakiwa kulipia, lakini kwenye ADR hakuna gharama na inapunguza mrundikano wa kesi mahakamani.





# Wafariki dunia kwa kula uyoga wenye sumu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATU wawili wa familia tofauti, wakazi wa Mabatini wilayani Nyamagana mkoani Mwanza, wamefariki dunia huku wengine saba wakiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani Kanda Bugando baada ya kula uyoga unaosadikiwa kuwa na sumu.

Watu hao wanadaiwa kununua mboga hiyo juzi katika genge moja lililoko jirani na makazi yao ikiwa ni kawaida yao kufanya hivyo bila kupata madhara yoyote.

Akithibitisha kutokea kwa vifo hivyo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, alitaja waliofariki dunia kuwa ni Maua Mwilikwa (10) ambaye umauti ulimkuta akiendelea kupatiwa matibabu hospitalini hapo majira ya saa 11 alfajiri.

Mwingine ni Thomas Thomas (18) aliyefariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Sekou-Toure majira ya saa nane mchana.

“Watu saba kutoka familia ya Eva Jonas (47) wa Mabatini Mashariki baada ya kuanza kuharisha na kutapika walikimbizwa katika kituo cha afya cha Polisi Mabatini ambapo baada ya hali zao kutoridhisha walipelekwa katika Hospitali ya Sekou-Toure kwa matibabu zaidi na Thomas alifikwa na umauti hospitalini hapo,”alisema SACP Mutafungwa.

Aidha alitaja wanaoendelea kupatiwa matibabu kuwa ni Maua Ibrahimu (56), Eva Jonas (47), Edina Thomas (20), John Thomas (15), Tomision Thomas (13) mwanafunzi wa kidato cha kwanza shule ya sekondari Mtoni, Grelious Simoni mwaka mmoja na Alfani Selemani (14) na hali zao zinaendelea vizuri.

Hata hivyo alisema jeshi hilo linaendelea kumtafuta mtu aliyewauzia uyoga huo ili aweze kuhojiwa na kueleza aliutoa wapi na kutoa rai kwa wananchi kuwa makini na baadhi ya vyakula visivyofaa.



Baadhi ya waandishi wa habari kutoka mikoa ya Geita, Simiyu, Tabora na Shinyanga, wakiwa kwenye mafunzo yaliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuhusu usambazaji na uhamasishaji wa matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi 2022 jana mkoani Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Milioni 964/- zaboresha huduma ya elimu Nzega

**Na Halima Ikunji,** NZEGA

ZAIDI ya Sh. milioni 964 zimetumika katika ujenzi wa shule mbili za sekondari na msingi katika Kata ya Mwasala, Halmashauri ya Nzega mkoani Tabora na kuondoa kero zilizokuwa zikiwakabili wanafunzi wa eneo hilo.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo, ofisa mipango wa halmashauri hiyo, James Raymond, alisema ujenzi wa shule za sekondari uligharimu Sh.milioni 603 na shule mpya ya msingi Mwandu ambayo imegharimu Sh.milioni 331.

Alisema hali hiyo umewaondolewa wanafunzi adha ya kutembea zaidi ya km 20 kufuata masomo katika kata ya jirani na kusababisha wengi wao kushindwa kuendelea na masomo.

“Zaidi ya nusu ya wanafunzi walikuwa wakishindwa kumaliza masomo ya darasa la saba huku kati ya wanaohitimu walishindwa kuendelea na masomo ya sekondari kutokana na shule kuwa umbali wa zaidi ya km 20,” alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwasala, Jonas Kwiyera, alisema wastani wa watoto 50 hadi 100 walikuwa wanaacha shule kila mwaka kutokana na kutembea umbali mrefu na kuvuka mto ambao ulikuwa hatari kwao. “Mfano kati ya wanafunzi 320 walioanza darasa la kwanza mwaka 2017 shuleni kwetu ambao waliomaliza darasa la saba ni 147 tu, hivyo tunashukuru serikali kwa kupata shule hii mpya kwani watoto wengi wanaotoka kijijini hapa ndio wanaongoza kwa kuacha shule,”alisema Mwl. Jonas.

Naye Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Nzenga, Magesa Mgeta, alisema ujenzi wa shule hiyo mpya umesaidia kudhibiti utoro kwani hali ilikuwa mbaya ambapo kwa mwaka huu kati ya watoto 187 walioanza kidato cha kwanza mwaka jana waliofanya mtihani wa kidato cha pili ni watoto 47.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Modest Apolinary, alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake njema ya kumaliza kero za wananchi katika sekta zote kwa halmashauri hiyo.

Alisema halmashauri hiyo imepokea zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya halmashauri na Sh. bilioni moja za ujenzi wa hospitali mpya katika kijiji cha Lubisu Kata ya Utwigu na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba.

## Viongozi wanaotishia waandishi waonywa

**Na Waandishi Wetu**

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi nchini mwaka 2022, Anne Makinda, amewaonya wakuu wa mikoa na wilaya kuacha tabia za kuwatishia waandishi wa habari wanaoibua habari zinazogusa matatizo ya wananchi katika jamii kupitia takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wanahabari kutoka mikoa ya Geita, Shinyanga, Simiyu na Tabora juu ya usambazaji na matumizi ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Alisema serikali inafanya sensa ikiwa na lengo la kujua wananchi, miundombinu pamoja na rasilimali walizonazo hivyo ni jukumu la wakuu hao kutoa ushirikiano kwa waandishi katika upatikanaji wa taarifa sahihi.

Vilevile aliwataka kuacha kuficha takwimu ambazo vyombo vya habari vinahitaji kwa lengo la kuhabarisha umma juu ya jambo fulani, kwani hata takwimu za kuandikisha wanafunzi wa awali na darasa la kwanza imekuwa tatizo kutolewa.

Mratibu wa Sensa Mkoa wa Shinyanga, Eliud Kamendis, akitoa taarifa ya sensa alisema, awamu hii ni ya mwisho na inajumuisha uchakataji, utambuzi, uandishi wa ripoti pamoja na usambazaji.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Shinyanga (SPC), Greyson Kakuru, alisema, mafunzo hayo yatawasaidia waandishi wa habari kuandika habari kwa usahihi na kuepuka upotoshaji ambao umekuwa ukijirudia.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akifungua mafunzo hayo alisema, ofisi yake imekuwa ikitoa ushirikiano kwa wanahabari juu ya utoaji wa takwimu na pale wanapoibua changamoto kwenye jamii amekuwa akifika na kutatua.

Alitoa maelekezo kwenye ofisi nyingine kutowabagua na kuwakwamisha waandishi pale wanapohitaji kupata habari au takwimu za awali na kuwataka kutumia kikamilifu matokeo ya sense kuuhabarisha umma.

**Imeandaliwa na Shaban Njia, Marco Maduhu (SHINYANGA).**

**Mratibu wa Sensa Mkoa wa Shinyanga, Eliud Kamendis, akitoa taarifa ya sensa alisema, awamu hii ni ya mwisho na inajumuisha uchakataji, utambuzi, uandishi wa ripoti pamoja na usambazaji.**

Ukurasa 13



Watanzania wanaposubiri CHADEMA kutekeleza amri ya Mahakama Kuu

Ukurasa 1 4



**USHINDI WA ABDEL FATTAH al-SISI**
**Vita Hamas, Israel ilivyomjengea imani, Misri wamchagua wakimwamini kiulinzi**



# Rwanda, Kenya kuondoa viza ni sawa, huenda Tanzania ikafaidika

## • Wengi kuja kuona Mlima Kilimanjaro

**Na Sabato Kasika**

RWANDA haina mipaka kwa Waafrika, imeondoa masharti kwa wanaotaka kuingia nchini humo wasijisumbue kupata visa.

Hatua hiyo ni mwanzo wa kuunga mkono makubaliano ya Umoja wa Afrika (AU) ya 'Agenda 2063' ya kuwa na Afrika isiyo na mipaka iliyotengamana kwa hali zote.

AU kupitia Ajenda 2063 au 'the Africa we Want', ina maono ya kufikia bara lenye msukumo mpya linalotumia sarafu na pasi moja, lisilo na mipaka kila mmoja akiishi na kutembea apendavyo, tena likiongozwa na serikali moja chini ya mtangamano madhubuti.

Rwanda inaanza kuondoa vikwazo vya usafiri kwa Waafrika wakialikwa kupanda ndege kwenda Rwanda wanapohitaji.

Wakati Rwanda ikiwa tayari imeshatangaza hatua hiyo kwa Waafrika, Kenya nayo inasema, inatarajiwa kuwa nchi isiyo na viza kwa yeyote kuanzia mwezi ujao.

Ni kauli ya Rais William Ruto, wakati wa maadhimidho ya siku ya Uhuru wa Kenya, kwamba hatua hiyo ni kutimiza ahadi ya kukomesha hitaji la wasafiri wanaoomba viza kuzuru Kenya.

Rwanda na Kenya ni miongoni mwa nchi nane zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), za Tanzania, Congo DR, Uganda, Burundi, Somalia na Sudan Kusini ambazo hazijatangaza uamuzi kama huo.

Nipashe inazungumza na baadhi ya wachambuzi wa mambo ya diplomasia na wadau wengine, ili kupata maoni yao kuhusu hatua hiyo na umuhimu wake na athari zake kwa jumuiya.



Dorothy Semu Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Tanzania Bara. **PICHA: MTANDAO**

Abbas Mwalimu ni Mdhahiri wa Chuo cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam, ambaye anasema, suala la Rwanda na Kenya kutangaza utaratibu wa raia wa kigeni kuingia kwenye mataifa hayo bila viza, linaweza kuwa na sura mbili za faida na hasara.

"Labda Kenya inasema, inafanya hivyo ili kuvutia watalii, waweze kufika kwa wingi na hivyo inaweka mazingira ya kuwavutia, kwani imekuwa ikisema karibu Kenya uone Mlima Kilimanjaro," anasema.

Aidha, ni kweli mtalii akiingilia Kenya unauona mlima lakini ili aufikie lazima aje Tanzania, na kwamba kuondoa viza kunaweza kuvutia watalii wengi kufika nchini humo na kuingiza fedha nyingi za kigeni, ingawa wakitaka kufika Mlima Kilimanjaro lazima watakuja Tanzania.

"Kwa njia hiyo Kenya watakuwa wamefaidika zaidi. Vilevile ukiangalia ripoti za hivi karibuni, ukiacha Morocco, Tanzania imekuwa ya pili kwa Afrika kwa kuvutia watalii wengi, hivyo na Wakenya nao wanatafuta kila mbinu za kuwapata," anasema Mwalimu.

Pamoja na mbinu hiyo, Mwalimu anasema ana mashaka na utaratibu huo wa kuondoa viza kwamba unaweza kuchangia hata wahalifu kupata mafichо na kuhatarisha usalama wa EAC

"Unaporuhusu kila mtu kuingia nchini kwako, unaruhusu hata wahalifu kuingia kwa sababu hawahitaji kutumia njia za panya japo si wakati wote. Sasa ni kwa kiasi gani Kenya imetengeneza mazingira ya kuhakikisha usalama wake unakuwa ni kipaumbele...? Anahoji.

### USALAMA KWANZA

Mchambuzi wa masuala la siasa na Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, anasema kuwa mwanachama EAC, , hakuzuii nchi kujiamulia mambo yake yenyewe ambayo inaona yanafaa.

Hata hivyo anatoa angalizo:"Nchi hizo zilizoamua kuondoa viza ni nchi huru zina uhuru wa kujiamulia mambo yake yenyewe bila kuingiliwa na nchi nyingine Kwa maslahi ya nchi zenyewe kama zinaona kuna fursa. '

Aidha, anasema jambo la muhimu zaidi ni usalama, hasa kwa kuzingatia kwamba kuna tatizo la ugaidi na uasi Afrika na duniani, wahalifu wanaweza kutumia nafasi hiyo kuhatarisha usalama wa taifa.

"Usalama wa nchi hizo na hata zile ambazo ziko ndani ya jumuiya unaweza kuwa hatarini, ila kama suala la usalama limechambuliwa kwa kina hadi zikafikia hatua ya kuruhusu watu kutoka mataifa mengine kuingia bila viza, sina tatizolakini kama bado kuna haja ya kutafakari," anasema Wangwe.

Kadhalika, Wangwe anasema, kama nchi haijajipanga, inawezekana fursa zote za nchi zilizoruhusu kuingia bila viza zinachukuliwa na wageni na kusababisha wenyeji kubaki hawana kitu.

Wangwe anasema, taifa kuwa na utaratibu huo wa bila viza, ni njia mojawapo ya kutafuta wawekezaji, kwa kuwa inakuwa ni fursa kuwafikia wengi na kupata fedha za kigeni ili kuinua uchumi wake.

"Ila suala la usalama wa nchi na hata zilizo ndani ya jumuiya ni la msingi, lakini pia wageni wasije kuchukua fursa zote na kuwaacha wenyeji wakiteseka," anasema.

### UAMUZI CHANYA

Makamu wa Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Tanzania Bara, Dorothy Semu, anasema uamuzi huo ni chanya, hasa kwa kuzingatia kwamba nchi za Afrika Mashariki ina watu zaidi ya milioni 300 na ongezeko la watu wa kipato cha

INAENDELEA UK. 14

## MATAJIRI WA DUNIA 2023

# Marekani yaendelea kushikilia usukani

**Na Mwandishi Wetu**



Tajiri namba 4 Bill Gates

Aliko Dangote bilionea wa kwanza Afrika.

MO Dewji, bilionea namba 15 Afrika

Bilionea wa dunia Elon Musk,

WAKATI mwaka 2023 ukielekea ukingoni suala la rasilimali na utajiri linaendelea kuigawa dunia, ambayo ina makundi mawili ya matajiri au mabilionea na walalahoi au mafukara wanaopatikana kusini ya dunia.

Hadi mwaka unapoyoyoma Marekani ndiyo nchi yenye matajiri wakubwa duniani, ikiwa na karibu mabilionea wote wa sasa.

Leo mtu tajiri zaidi duniani ni Elon Musk (52), ambaye utajiri wake ni dola bilioni 222. Musk alinunua kampuni ya Twitter Oktoba 2022 kwa Dola bilioni 44. Na sasa imepewa jina la X.

Mwamerika mwingine Jeff Bezos (59), anashikilia nafasi ya pili kwa utajiri zaidi duniani, akimiliki kampuni ya biashara mtandaoni ya Amazon (AMZN). Utajiri wake una thamani ya Dola bilioni 171 ni kwa mujibu wa gazeti la The Forbes.

Tajiri namba tatu duniani ni Bernard Arnault (74) anayeishi Ufaransa. Ni mtu maarufu akimiliki kampuni ya LVMH (LVMUY). Thamani ya utajiri wake ni Dola bilioni 169 akiwa na hisa kubwa ya umiliki sawa na asilimia 97.5 ya kampuni ya Christian Dior.

Aidha, Bernard Arnault ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni kubwa zaidi ya bidhaa za anasa au kifahari duniani "Moet Hennessy Louis Vuitton (LVMH)" ikizalisha bidhaa maarufu za mitindo ya mavazi, vipodozi, manukato, marashi na vito kutoka kampuni ya vito vya Tiffany & Co.

Bill Gates, anashikilia nafasi ya nne kwa utajiri zaidi duniani. Gates (68) anaishi Marekani, akifahamika kuwa mwanzilishi mwenza wa kampuni ya kompyuta ya Microsoft (MSFT.

Bilionea huyu utajiri wake unafikia Dola bilioni 134. Ni maarufu kuchangia maendeleo kwa maskini wanaoishi kizio cha kusini ya dunia ambao ni pamoja na Afrika na Asia, akisaidia fedha za kupambana na magonjwa na kuendeleza matumizi ya TEHAMA.

Bill Gates ndiye mmiliki mkubwa zaidi wa mashamba nchini Marekani na amewekeza katika kampuni mbalimbali kama reli huko Canada na AutoNation.

Akiwa na miaka 79, Larry Ellison, ni wa tano kwa utajiri duniani, akitokea Marekani. Ni mmiliki wa kampuni ya Oracle (ORCL), akijivunia utajiri mkubwa wa Dola bilioni 129.

Steve Ballmer (67) mmiliki wa Los Angeles Clippers ni wa sita kwa utajiri duniani utajiri wake ukifikia dola bilioni 129.

Ballmer ni mfanyabiashara na mwekezaji wa Marekani ambaye aliwahi kuwa ofisa mkuu mtendaji wa Microsoft kuanzia 2000 hadi 2014. Yeye ndiye mmiliki wa Los Angeles Clippers, timu ya mpira wa kikapu.

Mkongwe akiwa na miaka 93 ni Mwamerika Warren Buffet, Mkurugenzi Mtendaji wa Berkshire Hathaway (BRK.A) inayojihusisha na mitaji, uwekezaji kwenye bima na kwa ujumla fedha, ni wa saba kwa utajiri duniani, wenye thamani ya dola bilioni 119.

> 'Kadogoo' kiumri si kipesa, Mark Zuckerberg mwenye umri wa miaka 39 na anayeishi Marekani pia anashikilia namba tisa. Ni Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa Meta Platforms (META), akikusanya utajiri mkubwa wa dola bilioni 115.

Larry Page (50) anayepatikana pia Marekani, anasimama kama mwanzilishi mwenza na mjumbe wa bodi ya Alphabet (GOOG), akijivunia utajiri mkubwa wa dola bilioni 119.

'Kadogoo' kiumri si kipesa, Mark Zuckerberg mwenye umri wa miaka 39 na anayeishi Marekani pia anashikilia namba tisa. Ni Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa Meta Platforms (META), akikusanya utajiri mkubwa wa dola bilioni 115.

Meta Platforms imejikita katika tasnia ya teknolojia ya mitandao ya kijamii ikiwa miongoni mwa waanzilishi wa face book.

Mwanzilishi mwenza na mjumbe wa bodi ya Alphabet (GOOG), Sergey Brin (50) anayeishi Marekani, ana utajiri mkubwa wa dola bilioni 113. Anasifika kusimamia kimkakati utajiri wake, pamoja na mali muhimu kama dola bilioni 16.4 taslimu, anazomiliki.

Brin ni mwanzilishi mwenza wa Google na Larry Page, aliwahi kuwa rais wa kampuni kuu ya Google, Alphabet Inc hadi alipojiuzulu Desemba 2019.

**MATAJIRI AFRIKA**

Licha ya mabilionea wengi duniani kuwa Waamerika wanaoishi wakipatikana Marekani, Afrika nayo ina vigogo wenye utajiri mkubwa wanaoishi barani humu wakiongozwa na Mnaigeria Aliko Dangote (65).

Akiwa na utajiri wa Dola bilioni 13.5, Dangote anajivunia uwekezaji katika sementi na sukari kuwa ndicho kilichompa utajiri huo.

Pamoja naye ni bilionea namba mbili Johann Rupert (72), raia wa Afrika Kusini. Anamiliki utajiri wa dola bilioni 10.7, ambao ni uwekezaji wa bidhaa za kifahari (luxury goods).

Namba tatu ni Niccky Oppenhrmrt (77) ni bilionea anayeshikilia kibindoni dola bilioni 8.4, mali ikichumwa kutoka kwenye uwekezaji mkubwa wa almasi duniani.

Namba nne ni Abdulsamad (62), akiwa na dola bilioni 7.6. Huyu ni Mnaigeria ambaye naye ametajirika kupitia uwekezaji kwenye sementi na sukari.

Bilioni mwingine anayefuata ni Nassef Sawiri (62) tajiri mkubwa anayemiliki mali kutoka kwenye uwekezaji wa tasnia ya ujenzi na ukandarasi. Raia huyu wa Misri ana utajiri wa dola bilioni 7.2.

Bilionea mwingine barani Afrika ni Mike Adenuga (69) mwenye utajiri wa dola bilioni 5.6 akitajirishwa na uwekezaji kwenye tasnia ya teknolojia ya mawasiliano na simu pamoja na uzalishaji mafuta yenye viwango na ubora huko Nigeria.

**KUSINI YA SAHARA**

Bilionea namba tisa Afrika ni Patrice Motsepe (60), ambaye ni Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Mzaliwa wa Afrika Kusini ana utajiri wa dola bilioni 3.1 akiwekeza kwenye madini na shughuli nyingine zinazohusiana na vito.

Tanzania ni sehemu ya mabilioni wa Afrika, Mohamed Dewji (47) almaarufu 'MO DEWJI', anashikilia namba 15 ya mabilionea Afrika.

Aidha, anatajwa kuwa miongoni mwa mabilionea vijana Afrika mwenye utajiri wa dola bilioni 1.5.

Ni mmiliki wa kampuni ya MeTL anayowekeza kwenye maeneo mbalimbali kuanzia uzalishaji wa nguo, vinywaji, unga na mafuta ya kula. MeTL inafanyabiashara kwenye mataifa mengi hasa ya Kusini na Mashariki mwa Afrika.

Aidha, ni mwekezaji mkuu wa Klabu ya Simba

**TAARIFA HIZI NI KWA MUJIBU WA JARIDA LA FORBES LA MAREKANI.**

# Watanzania wanaposubiri CHADEMA kutekeleza amri ya Mahakama Kuu

**Na Ani Jozeni**

NI mara ya pili ndani ya mwaka mmoja kwa taasisi za dola, kutatua migogoro ndani ya vyama vya siasa ambayo havikuwa na uwezo wa kuitatua wao wenyewe kwa njia inayoridhisha na yenye uwezo wa kisheria.

Uamuzi wowote wa kijamii, kisiasa au kibiashara ambao unagusa maslahi muhimu ya baadhi ya watu inabidi uwe na uwezo wa kuheshimiwa na vyombo vya utawala, kwa kanuni ambazo wanazifahamu.

Vyombo vya nchi mara nyingi haviwi mwamuzi wa kati ila vinakuwa na sura ya mchezaji wa ziada anayefunga dakika za majeruhi watu wanapochoka.

Ziko pande mbili za uchovu ambao unatumiwa na vyombo vya dola kumaliza ubishi katika vyama vya siasa, kutokana na hali ya mivutano ndani ya vyama hivyo huwapo maamuzi ambayo yanakidhi haja za wanaoviongoza.

Yako mazingira ambako maamuzi yao yanapingwa katika makundi mapana ya jamii ambayo hayana uwezo wa kuingilia kati maamuzi ya kamati za juu au mabaraza tendaji ya vyama vya siasa.

Yule mchezaji wa ziada, vyombo vya dola, anapopelekewa suala hilo anajua ni kitu gani hasa, au uamuzi gani maridhawa unangojewa na makundi ndani na nje ya chama.

Ndiyo maana kwa viongozi wa vyama vya siasa waliopo madarakani wakati wowote ule, vyombo vya dola huwa vinawaharibia mipango yao vikianza kupelekewa masuala ambayo kimsingi yalitakiwa yaishie ndani ya chama, hata kama si kutatuliwa kwa maana ya kufikia muafaka au makubaliano. Na mpaka suala lolote lifike mahakamani ina maana kuwa vikao vyote vinavyohusika vimeshindwa, na hadi sasa masuala yanayofika hapo ni yale ya vyama vya upinzani, kwani maamuzi ya chama tawala huwakilisha dola.

Chini ya mifumo ya kisheria iliyopo, hakuna uamuzi wa Kamati Kuu CCM unaoweza kufikishwa mahakamani, kwani mwenyekiti wa kamati hiyo ndiye mkuu wa dola.

Ndiyo maana kwa upande mwingine inaonekana kama ni chama tawala ndicho kinaamua masuala nyeti katika vyama vingine vya siasa, kutokana na kutumia mfumo wa dola ambao ni mtiifu kwa hisia, siyo tu matakwa, ya CCM kama chama tawala.

Licha ya kuwa kwa mifumo ya vyama kuna chembe ya ukweli, bado inabakia kuwa mifumo ya sheria au mahakama ni kimbilio la wapinzani wanapokuwa 'mguu upande' na viongozi wao, na ndicho kilichotokea katika mivutano NCCR-Mageuzi, na sasa CHADEMA.

Ni mazingira ambayo yanavuruga mwelekeo wa uongozi kuhusu suala fulani, kushindwa kulisimamia.

Ndiyo hapo linaingia suala la uchovu katika 'mustakabali' wa maamuzi kama hayo, kuwa una sehemu mbili, iwe ni kuchokwa kwa viongozi kama James Mbatia aliyekuwa Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, bila kuwa na njia ya kumwondoa madarakani kwa kutumia taratibu anazozifahamu, ambazo angeziheshimu, akakubali kushindwa.

Katika suala la CHADEMA, hapakuwa na aliyetinga mahakamani baada ya uchaguzi mkuu wa ndani ya chama bali baadhi ya wasioridhika na uendeshwaji wake, au matokeo yake, walirudi CCM kama 'chama mama.' Au kwa lugha ya kawaida ni kama 'walirudi nyumbani,' si kuasi.

Kuchoshwa kwa maana nyingine ni watu kutokuwa na hamu ya kusikiliza tena mdahalo kuhusu suala la wabunge 19 wa Viti Maalum, na hivyo ukitokea uamuzi dhidi ya uongozi wa juu wa chama hicho katika suala hilo hautaamsha hamasa yoyote ile katika jamii.

Ni mbinu ya kawaida ya 'mahakama jamii' ambayo inatumiwa kwa kina kuondoa matatizo ndani ya mfumo wa dola, pale watendaji waandamizi wanapokabiliwa na madai ya ubadhirifu wa fedha za umma (kukwepa neno wizi), wakamatwe na kubakia ndani (kwa mfano kwa masuala ya uhujumu uchumi) hasa kwa mwaka mmoja, au zaidi. Mwishowe kesi hiyo inafutwa kwani Mkurugenzi wa Mashtaka hawezi kuitisha ushahidi mahakamani ambao unaweza ukaiaibisha dola, hivyo inakuwa bora aachane na kesi hiyo.



Wabunge 19 wa viti maalumu CHADEMA, ambao tangu 2020 wamekuwa gumzo la kukataliwa ubunge wao na hata kuvuliwa uanachama. **PICHA MTANDAO**

> Uchovu huo unaendana na muda ambayo tayari umepita tangu suala hilo lifumuke mwisho wa mwaka 2020, na sasa ni 'lala salama' ya mwaka 2023, hivyo ni miaka mitatu kamili mgogoro huo unafukuta.

Uamuzi kuhusu ubunge Viti Maalum wa wana-CHADEMA 19, vinara wa Baraza la Wanawake la BAWACHA hadi mgogoro huo ulipofumuka, uliosababisha kubandika jina la fedheha la 'COVID-19,' ni mjumuisho unaoweka pamoja uamuzi dhidi ya vikao vya juu vya CHADEMA kama ilivyokuwa kwa NCCR-Mageuzi (kubariki vikao dhidi ya mwenyekiti wa chama).

Ila tofauti na uamuzi huo dhidi ya Mbatia, huu ulichelewa sana, hadi hata suala la kupiganiwa kama sehemu ya maslahi halisi au muhimu ya chama kuanza kufifia.

Hivyo badala ya kuwa uamuzi wa kubatilisha yaliyofikiwa katika vikao vya juu vya CHADEMA, uamuzi wa Mahakama Kuu si pigo , kwanza kuwapa zawadi makundi ya wanaharakati na wajinsia wanaotaka 'COVID-19' wabaki bungeni, halafu na dhamira ya dola ya kuhakikisha matokeo ya uchaguzi mkuu 2020 yanaheshimiwa, na mapungufu yake yajadiliwe katika kuandaa uchaguzi mkuu unaofuata.

Uchovu huo unaendana na muda ambayo tayari umepita tangu suala hilo lifumuke mwisho wa mwaka 2020, na sasa ni 'lala salama' ya mwaka 2023, hivyo ni miaka mitatu kamili mgogoro huo unafukuta.

Kwa vile kuna chembe za uliberali katika masuala ya sheria na haki za vyama vya siasa, uhuru wa kufanya mikutano (mradi kusiwe na tahadhari ya kuhamasisha maandamano au ushawishi kama huo), baadhi walitazamia kuwa huenda katika hili mahakama ikawa na 'ubavu' wa kubatilisha maamuzi ya dola dhidi ya chama.

Ambacho mwelekeo huo haukuangalia ni hisia za jamii kubwa kwani kuna fikra kama ile ya wanamichezo, ambako kuna kundi la soka linatambulishwa kama 'wananchi,' na hivyo katika siasa CHADEMA inatambulisha dhamira ya madaraka kuwa ni ya 'watu.'

Lipo eneo jingine ambalo viongozi wa CHADEMA wakashindwa kukiri kuwa ni sehemu ya 'pigo' kuwa hata wao hawana malashi ya kuendeleza ugomvi huu ambao katika mazingira ya sasa unaweza tu kuendeleza malumbao, si kupata uungwaji mkono.

Licha ya kuwa katika uanaharakati au mapambano kuhusu uchaguzi mkuu 2020 hatua ya kuwavua uanachama kutokana na kukaidi amri ya chama ya kususia bunge ilikuwa haikwepeki, nje ya Kamati Kuu kujivua uwezo wa kufanya maamuzi hayo, sasa ni wakati wa kuweka pembeni tofauti hizo, na ikiwezekana hata hao 19 waipigie debe CHADEMA uchaguzi ujao.

Tuone kama Baraza Kuu litatii amri ya mahakama juu ya ushiriki wa wajumbe wanaoelezwa kuwa walifanya maamuzi ya kuwavua uanachama na pia kuwa sehemu wajumbe wa Kamati Kuu iliyowavua uanachama huo.

USHINDI WA ABDEL FATTAH AL-SISI

# Vita Hamas, Israel ilivyomjengea imani, Misri wamchagua wakimwamini kiulinzi

**Na Christina Mwakangale**

ABDEL Fattah al-Sisi (69), amekilinda kiti cha urais nchini Misri, kwa ushindi wa asilimia 89.6 katika kura zilizopigwa, dhidi ya wapinzani wake.

Mamlaka ya Uchaguzi Misri (NEA), juzi Jumatatu imemtangaza Rais al-Sisi, kuwa mshindi wa uchaguzi uliopita kwa kupata asilimia 89.6 ya kura, inaripoti Radio ya Ufaransa rfi, ikiongeza kuwa anaingia muhula wa tatu na kwa mujibu wa katiba ya Misri, ataongoza kwa miaka sita.

Katika uchaguzi wa 2014 na 2018, al-Sisi alishinda kwa zaidi ya asilimia 96 ya kura, hivyo ushindi wa mwaka huu unaonyesha kushuka kwa asilimia karibu 10, rfi inaripoti.

Wapinzani wake wameukataa ushindi wake licha ya kwamba, NEA imemwashia taa ya kijani, waliochuana naye ni pamoja na Farid Zahran anayekiongoza Chama cha Social Democratic.

Mwingine ni Abdel-Sanad ambaye ni kiongozi wa chama cha Liberal Wafd na mwanzilishi wa chama cha Kiliberali cha People's Republican.

Taarifa kuhusu ushindi huo, zimetolewa jana katika tovuti ya kituo cha habari Reuters, huku mgombea mmojawapo akiambulia asilimia 4.5 ya ushindi, huyo ni Hazem Omar, wa chama cha Republican People's Party.

Wamisri zaidi ya milioni 39 walimpigia kura Sisi, mkuu wa jeshi wa zamani ambaye amekwishatawala nchi hiyo ya kiarabu kwa muongo mmoja sasa, inaripoti tovuti ya CNN ya Marekani.

Uchaguzi huo, umefanyika huku ukitajwa na wachumi kwamba Misri inapitia kipindi kigumu cha uchumi, ikijaribu kujilinda na athari zitokanazo na kinachoendelea huko Ukanda wa Gaza.

Misri, inachangia mpaka kati yake na Palestina wenye kilomita 12 na Wamisri wengi wamehamasika kumpigia al-Sisi kura ili aendelee kulinda amani ya taifa hilo kutokana na sera zake.

Wapigakura baadhi yao wanasema kuibuka kwa mgogoro kwenye ukanda huo, kuliwashawishi kumpigia kura Sisi.

Wanasema ni kiongozi ambaye mara kadhaa amejitambulisha kama ndiye ngome na utulivu wa nchi hiyo.

Jambo hilo, limekuwa dhahiri na amekuwa akiungwa mkono na nchi za ukanda huo wa Kiarabu pamoja na mataifa Magharaibi pia zikivutiwa kuelekeza misaada kwa serikali yake, inaripoti CNN.



Abdel Fattah

Mchakato wa uchaguzi nchini humo ulikuwa wa siku tatu, kuanzia Desemba 10 hadi 12, mwaka huu.

Mamlaka ya uchaguzi nchi humo inasema imerekodi mafanikio ya uchaguzi huo kwa asilimia 66.8, ikiwa ni juu yarekodi ya uchaguzi uliopita wa mwaka 2008 ikiwa ni asilimia 41.

Uchaguzi huo ulishirikisha wagombea wa kiti cha urais watatu, ingawa hakukuwa na hata mmoja wao aliyekuwa na hadhi ya juu.

Mpinzani mashuhuri zaidi alijitoa katika uchaguzi huo Oktoba, mwaka huu, akisema maofisa na wahalifu waliwalenga wafuasi wake.

Hata hivyo, shutuma hizo zilitupiliwa mbali na Mamlaka ya Taifa ya Uchaguzi.

"Kulikuwa hakuna uchaguzi, al-Sisi anatumia serikali yake kama nyenzo na alivitumia vyombo vya ulinzi ili kuzuia ushindani katika mbio za kuwania kiti chake," anasema Hossam Bahgat, Mkuu taasisi ya kutetea haki ya Egyptian Initiative for Personal Rights (EIPR).

"Ni kama wakati uliopita aliwachagua wapinzani wake ambao waliingia tu kwa hoja za kugombea urais kimya kimya, bila kukosoa sera zake mbaya," anaongeza Bahgat.

Awali, ushawishi raia kupiga kura ulitumia njia ya televisheni, matangazo, vipindi vya mazungumzo na matangazo ya kizalendo.

**UONGOZI WAKE**

Mwaka 2013 jeshi likiongozwa na al- Sisi liliuangusha utawala wa rais aliyechaguliwa kidemokrasia Mohammed Morsi, aliyekuwa rais wa kwanza wa nchi hiyo baada ya ghasia za mwaka 2011, inasema DW.

Chini ya utawala wa al-Sisi, maelfu ya wanaharakati na wafuasi wa dini ya Kiislamu wamefungwa jela au kulazimika kuishi uhamishoni, kwa mujibu wa DW.

Aidha, inasema vyombo vya habari vimekuwa vikidhibitiwa kwa kiasi kikubwa na katika miezi ya hivi karibuni, serikali ya nchi hiyo ilikamata wapinzani kadhaa wa serikali.

Rais huyo, alichaguliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2014 na 2018, awamu zote akishinda kwa asilimia 97 ya kura zilizopigwa.

Katiba ya nchi hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2019, kuongeza muda wa urais hadi miaka sita kutoka minne na kuruhusu Sisi kugombea muhula wa tatu.

Wakazi wa Misri, baadhi wanastaajabia na kuvutiwa na serikali kwa ujenzi wa miundombinu ikiwa ni pamoja na mji mkuu mpya uliojengwa katika jangwa mashariki mwa Cairo.

Wengine wanaona kuupendezesha mji huo ni kama ubadhirifu wa gharama kubwa wakati ambao deni la ncji hiyo, limeongezeka na bei za bidhaa muhimu zikipanda, inaeleza DW.

Wafuasi wa al-Sisi wanasema, wanona umuhimu wa usalama ni jambo muhimu na kwamba baadhi ya makundi yamefaidika chini ya utawala wake.

Hali hiyo inajumuisha wanawake, anasema Nourhan ElAbbassy,msaidizi wa katibu mkuu wa tawi la vijana la chama kinachomuunga mkono al-Sisi, Homat AlWatan, kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters.

"Tungependa kuona wanawake zaidi wakishika nyadhifa muhimu, mawaziri wa kike katika baraza la mawaziri ili mradi tu wamehitimu.

"Na marekebisho ya sheria za haki binafsi ambazo zinahusiana na masuala kama vile ndoa, talaka na malipo ya pesa," anaongeza Nourhan.

Miongoni mwa Wamisri walionyesha kutojali kuhusu matokeo ya uchaguzi huo, wakidai matokeo hayo yalitarajiwa.

# RWANDA, KENYA KUONDOA VIZA NI SAWA, HUENDA TANZANIA IKAFAIDIKA

**INATOKA UK. 11**

kati.

Anafafanua kuwa wengi wao ndio wanaofanya utalii, biashara na kuongeza kuwa hatua hiyo ni faida kwa jumuiya na kwamba mipaka inapofungwa na kuweka vizuizi na kulazimisha mtu awe na viza, ni suala hasi linalozinyima nchi kuvuna kutoka kwa wanachama wengine.

"Rwanda imetoa ruhusa ya Waafrika wote kuitembelea bila kuhitaji viza. Mtu yeyote wa Afrika anaweza kuamka asubuhi akakata tiketi ya ndege akatembelea Rwanda na akafanya utalii na biashara kisha akaondoka bila kuulizwa viza. Huu ni uamuzi chanya," anasema Dorothy.

Anasema, Kenya nayo itaingia katika hali hiyo ya kutodai viza kwa mgeni yeyote ifikapo Desemba 30 mwaka huu, na kwamba nchi hizo zinafaa kuigwa kwa kuwa bara la Afrika linategemea mapato kupitia watalii.

"Hili ndilo lengo mojawapo la kuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, watu waweze kutembeleana, kufanya biashara, utalii na kuwa na mwingiliano wa kitamaduni, ili kuleta faida ndani ya nchi zetu wenyewe kwanza," anasema Dorothy.

Kiongozi huyo anasema, Tanzania nayo imeruhusu watu kutoka nchi ya DRC kuja hapa nchi bila kuhitaji viza, na kwamba nchi nyingine ambazo ziko ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki zingeiga mfano huo.



## HABARI DODOMA

# NBS: Singida si ya mwisho kiuchumi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imesema Mkoa wa Singida sio wa mwisho kwa uchumi kama inavyoelezwa na baadhi ya watu ikiwamo mitandao ya kijamii.

Mkurugenzi wa Takwimu za Uchumi kutoka NBS, Daniel Masolwa, akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) mwishoni mwa wiki alisema Mkoa wa Singida uko juu ya mikoa ya Simiyu, Songwe na Katavi.

Alisema taarifa zinazoonyesha kuwa Singida ni ya mwisho ni za muda mrefu tangu 2006 kwa sasa mkoa huo uko juu kiuchumi ukilinganisha na mikoa mingine.

Masolwa alisema ili kupata ukokotoaji mzuri unaoakisi pato la taifa la mkoa, takwimu za shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi zinatakiwa ziwe zinajitosheleza.

Alisema vigezo vinavyotumika kukokotoa pato la taifa unazingatia miongozo ya Umoja wa Mataifa (UN) lakini kikubwa kuwe na utaratibu unaofanana kwa kuwa takwimu zinazalishwa kati ya mkoa na mkoa, nchi na nchi.

Naye Mtakwimu kutoka NBS, Dk. Mwinyi Mwinyi, alisema kulingana na Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika 2022, uwiano wa umri tegemezi unaonesha Mkoa wa Singida wategemezi ni 106 katika kila watu 100 walio kwenye umri wa kufanya kazi.

Alisema uwiano wa umri tegemezi ni mkubwa zaidi katika halmashauri za Mkoa wa Singida ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa kila watu 100 wenye umri wa kufanya kazi.

Dk. Mwinyi alisema Halmashauri ya Manispaa ya Singida ina wategemezi wachache zaidi ya halmashauri nyingine ambao ni 82, Ikungi ni 114, Halmashauri ya Singida DC ni 113, Itigi 114, Manyoni 109, Makalama 106 na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba wategemezi ni 103 katika kila watu 100 wenye umri wa kufanya kazi.

"Uwiano wa umri tegemezi ni mkubwa sana katika Mkoa wa Simiyu ambao wategemezi ni 119 kwa kila watu 100 wenye umri wa kufanya kazi ukifuatiwa na Tabora na Katavi kila mmoja wategemezi ni 110," alisema.

Uwiano huo uliwashtua wajumbe wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa na kwamba kuna kazi ya ziada ya kufanya ili watu wafanye kazi kuongeza uzalishaji na mkoa kukua kiuchumi zaidi.

## Jaji Mkuu alia ushahidi kisayansi bado ni tatizo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Jumaa, amesema moja ya changamoto wanazokutana nazo wakati wa kusikiliza kesi mbalimbali ni ushahidi wa kisayansi dhidi ya watuhumiwa wa makosa mbalimbali hapa nchini.

Prof. Jumaa alibainisha hayo jana kwenye mkutano mkuu wa Chama cha Majaji Tanzania, uliofanyika jijini hapa na kuhudhuriwa na majaji wote pamoja na mahakimu.

Alisema ushahidi huo huwa ni mgumu sana kwa sababu watuhumiwa wengi wanakuwa hawaelewi na kusababisha kuwapa changamoto za majaji wanaosikiliza kesi mbalimbali.

Kutokana na hilo alisema wanapaswa kuweka mwongozo na mkakati wa kuhakikisha wanakabiliana na changamoto hiyo.

"Naomba mlifanyie kazi suala hilo kwasababu ni changamoto ambayo inasumbua majaji wengi kwenye utendaji wao wa kila siku," alisema Prof. Jumaa.

Alisema changamoto hiyo ni kubwa sana hivyo inapaswa kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili kuiondoa kero hiyo kwenye utendaji wao.

Aidha, alisema kuwa maoni ya wadau ni ya muhimu sana hivyo wanapaswa kuwasikiliza ili waweze kutenda haki wakati wa utendaji wao wa kila siku.

Kadhalika, alikitaka chama hicho kuwasambazia taarifa wanachama ikiwamo maandiko kwa wanachama ili waweze kusoma kilichoko.

Alisema wanapaswa kufanya kazi na wadau wengine wa Mahakama, hivyo jukumu lao ni kuona kama wengine wanavuka mipakani na wanapaswa kuwakumbusha.

Mwenyekiti wa Chama cha Majaji nchini, Jaji Mfawidhi John Kahyoza, aliwashukuru wanachama wote kwa kuhudhuria mkutano huo huku akiwasihi kusikiliza kwa makini ili waweze kuwa mabalozi wazuri.

Kahyoza, alisema mkutano huo wa mwaka ni muhimu kwa sababu utasaidia kuboresha mambo mbalimbali kwenye chama hiko na sehemu ya kazi.

Hata hivyo, alisema alisema kila mmoja anapaswa kuwa makini kusikilizwa na kwenda kuyafanyia kazi yale ambayo amefundishwa.



Katibu Tawala Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, Anjelina Marko, akitoa msaada wa vitu mbalimbali kwa ajili ya kinamama wazee wa mjini Mugumu juzi, ikiwa sehemu ya michango ya wafanyakazi wa Serengeti Serena Hotel kwa wasiojiweza ili kusherehekea sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watafiti waelekezwa kutatua changamoto katika jamii

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imeagiza watafiti nchini kufanya utafiti utakaokuwa suluhisho kwa matatizo mbalimbali katika jamii.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, wakati akitoa zawadi kwa watafiti walioshinda kwa kufanya utafiti bora.

Alisema miaka mitatu iliyopita walishindanisha watafiti ambapo wa kutoka Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Chuo cha Mandela walipata fedha kiasi cha dola milioni moja sawa na Shilingi bilioni mbili kwa kila taasisi kwa ajili ya kufanya utafiti.

"Safari hii tumepata jukwaa lile lile, tuna nchi 17 katika baraza la utafiti na tunawatafiti mbalimbali. Mfano utafiti wa SUA unaangalia usalama wa chakula kwa hiyo unaweza ukawa suluhisho kwenye nchi nyingine mfano Ghana, Congo au Zimbwabwe ambao ni washirika kwenye hili baraza," alisema.

"Tanzania tunavuna dagaa, Malawi kupitia Ziwa Nyasa wanavuna dagaa kwa hiyo inawezekana matokeo yake mpaka Malawi wakaomba huo utafiti kwa hiyo hii ni fursa ya kujiuza kwa sababu utafiti wao utakwenda kujadiliwa kwenye nchi 17,"alisema.

Dk. Nungu alisema kuwa utafiti utafanywa na taasisi nne kwa kuzingatia usawa wa jinsia ambapo watafiti wengi wamekuwa ni wanawake.

Alisema taasisi 32 za kitafiti zilishindanishwa ambapo nne pekee ndizo zilizoshinda na kila mtafiti anapewa Sh. milioni 120 kwa ajili ya kutekeleza utafiti huo na kwamba fedha hizo zimetolewa na serikali ya Uingereza.

Mtafiti mwandamizi katika Ofisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Alistida Mwijage, alisema wamepokea tuzo kutoka kwa Costech ili kuendeleza utafiti unaohusu kupunguza upotevu wa dagaa kwa kutumia nishati ya jua.

Alisema kuwa katika utafiti huo wanakwenda kuboresha uvumbuzi ambao ofisi yao washaufanya siku za nyuma katika Ziwa Tanganyika.

"Tulikuja na Soral Tent inayoweza kukausha samaki kwa wepesi na umakini katika majira yoyote iwe ya mvua au jua tutatumia huo uvumbuzi kuhakikisha unatumika pwani kwa sababu pwani kuna dagaa wakubwa wanaoendana na wale wa Ziwa Tanganyika," alisema.

Alisema kuwa uboreshaji wa mfumo huo utawashirikisha wavuvi wa maeneo husika ili kuzidisha usanifu.

Alifafanua kuwa wachakataji wakubwa wa samaki ni wanawake hivyo uvumbuzi huo utawasaidia kukuza kipato na kuwa na uhakika wa ajira.

"Wachakataji wakubwa wa dagaa ni wanawake kwa hiyo kwa kufanya hivyo tunakwenda kukuza kipato cha kinamama kwa kuzalisha dagaa bora wenye kuuzika kwa bei nafuu pia tunaongea uhakika wa ajira," alisema.

Naye Flex Nandonde Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) alisema kuwa wao kama Chuo cha Kilimo wameshiriki kwenye utafiti ambao ni kulipa thamani zao la mbaazi kwa kutengeneza uji na tambi.





# Kampeni vijana kupima VVU yaanzishwa Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMPENI maalumu ya kuhamasisha vijana kujitokeza kupima afya imeanzishwa mkoani Mbeya ikiwa ni sehemu ya mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na magonjwa mengine ya kuambukiza.

Kampeni hiyo ijulikanayo kwa jina la JIZINGATIE imeanzishwa na Taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya Afya Cheki kwa kwa kushirikiana na Shirika la HJFMRI ambapo vijana wanapatiwa elimu ya afya na kuhamasishwa kupima kwa hiari.

Mratibu wa Kampeni hiyo, Dk. Isaac Maro alisema kampeni hiyo itafanyika kwa siku tano jijini Mbeya na kwamba wanakusudia kuwafikia zaidi ya vijana 4,000 kwa kuwatembelea kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema vijana wanaolengwa na kampeni hiyo ni wale wenye umri wa kati ya miaka 15 na 35 ambao wanadaiwa kuwa wamekuwa wagumu kujitokeza kupima afya zao na kwamba kundi hilo ndilo hatarishi zaidi kwa maambukizi mapya.

Alisema wanawalenga vijana wanaopatikana kwenye vyuo mbalimbali mkoani humo pamoja na wale wanaopatikana mitaani wakiwa na shughuli mbalimbali."Tatizo ambalo lilikuwapo kwa muda mrefu ni vijana kutojitokeza kupima lakini kutokana na ubunifu tulioufanya kwenye kampeni hii vijana wengi wamejitokeza na matokeo tunayaona, tunaamini kwamba mpaka siku zote tano zinakamilika tutakuwa tumefikia lengo," alisema Dk. Maro.

Alisema kilichowapa mafanikio zaidi ni uwepo wa vijana wengi vyuoni pamoja hamasa ambayo imetolewa huku akisisitiza kuwa mbali na kupima maambukizi ya VVU pia wanapima na magonjwa mengine.

Baadhi ya vijana walisema wamekuwa wakishindwa kujitokeza kupima kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo vituo vya kutolea huduma kuwa mbali pamoja na woga wa kupokea majibu.

Mmoja wa vijana hao, Jackson Anangisye alisema vijana wengi huwa wanaogopa kupima kutokana na mienendo yao kutokuwa mizuri na hivyo huwa wanakosa kujiamini.

Alisema baadhi yao wanajihisi pengine watakuwa wamepata maambukizi kutokana na kushiriki ngono zembe na watu ambao hawawaamini.

"Hakuna kitu kigumu kama kupokea majibu ya vipimo vya Ukimwi, hata kama mtu njia zako siyo mbaya lakini kupokea majibu huwa ni kazi ngumu sana, inahitaji kujiamini sana," alisema Anangisye.

Mary Kaesya aliwashukuru wadau hao kwa kuwasogezea huduma hiyo pamoja na kutoa elimu akieleza kuwa vijana wengi wamekuwa wakishindwa kujitokeza kwa sababu huduma zinakuwa mbali na maeneo yao.

Alisema kampeni hiyo imesaidia vijana wengi kuhamasika kujitokeza kupima afya zao hali ambayo alisema itasaidia kupata takwimu sahihi za maambukizi ya VVU mkoani humo.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya, Mkoa wa Mbeya unashika nafasi ya tatu kwa maambukizi ukiwa na asilimia 9.6 ukitanguliwa na mikoa ya Iringa huku Mkoa wa Njombe ukiongoza kwa kuwa na asilimia 14.8.



Baadhi ya wajasiriamali wa mji wa Kiwira wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, wakiwauzia matunda abiria kwenye basi linalofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Wilaya ya Kyela hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC akemea madereva walevi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ametoa rai kwa madereva kuacha tabia za ulevi kwa sababu inaweza kuhatarisha maisha yao na ya abiria kwa kusababisha ajali ambazo zinaweza kuathiri watumiaji wengine wa barabara.

Rai hiyo ilitolewa wakati akifungua mafunzo kwa madereva na maofisa usafirishaji kutoka mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu yanayoendeshwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ambayo yanafanyika katika Halmashauri ya Mji Makambako mkoani humo.

Mtaka alisema madereva na maofisa usafirishaji walio kwenye ajira za serikalini na binafsi nchini pia wanapaswa kuzingatia maadili ya kazi yao pamoja na kuwa waaminifu ili kuepuka mambo yatakayoweza kusababisha kushusha heshima yao.

Alisema wapo madereva na maofisa usafirishaji ambao wamepitia mafunzo lakini wamekuwa wakishirikiana katika kuiba mafuta mambo ambayo ni ya ovyo na hayastahili kufanywa na wao.

"Yaani wewe dereva kabisa wa serikali na sekta binafsi umepewa gari umesoma chuo na una cheti chako, ofisa usafirishaji kasoma chuo mnatengeneza dili la kuiba mafuta ya gari la ofisini kwenu, tunakwambia peleka gari Temesa unashirikiana kuiba vipuri," alisema Mtaka.

Mtaka alisema ni lazima maofisa usafirishaji na madereva kuzingatia maadili ya kazi yao ili kuepuka fedhea ambazo hazina msingi wowote kwao.

Hata hivyo Mtaka alisema udereva ni taaluma kama zilivyo taaluma nyingine hivyo wanao wajibu wa kuhakikisha wanafuata miongozo yao.

Kaimu Mkuu wa Chuo Taaluma na Utafiti (NIT), Dk. John Mahona, alisema mafunzo hayo ya muda mfupi yatawaongezea madereva na maofisa usafirishaji kuwa umahiri katika kutumia ipasavyo vipuri vya magari na vilainishi pamoja na kufanya ukaguzi wa magari ili kuhakikisha matumizi sahihi ya mafuta, matairi na magari kwa ujumla.

Alisema pamoja na mafunzo ya madereva na maofisa usafirishaji pia kwa mara ya kwanza wamezindua kozi ya mafunzo ya ukaguzi wa barabara lengo ikiwa ni kuangalia usalama wa barabara.

Dk. Mahona alisema mafunzo hayo ni muhimu katika kuangalia usalama wa barabarani kwa watumiaji na wajenzi wa barabara ili kupunguza ajali za barabarani.

"Wahusika walioshiriki kwenye kozi hii mpaka sasa ni 27 ambapo wataalamu kutoka ofisi ya TARURA, TANROADS, LATRA, vikosi vya usalama barabani na mashirika binafsi kutoka ukanda huu wa nyanda za juu," alisema Dk. Mahona.

Kwa niaba ya madereva na maofisa usafirishaji walioshiriki mafunzo hayo, Musa Sabihi, aliahidi kuwa mafunzo watakayopata yatawasaidia wao katika kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa.

"Mkuu wa mkoa umeongea maneno machache lakini kama tutayashika yatatusaidia sisi na wengine katika kutekeleza majukumu yetu," alisema Sabihi.

# Watanzania washauriwa kutembelea vivutio utalii

**Na Nebart Msokwa,** NJOMBE

WATANZANIA wameshauriwa kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini kwa lengo la kujifunza vitu mbalimbali, kufurahia mazingira ya asili pamoja na kuiunga mkono serikali kwenye uhamasishaji wa watalii ili kuongeza pato la taifa.

Balozi wa Utalii nchini, Nangasu Werema, aliyasema hayo juzi alipotembelea Hifadhi ya Taifa ya Kitulo iliyopo mkoani Njombe ambayo imebatizwa jina la 'Bustani ya Mungu' kutokana na kupambwa na maua ya asili.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan alijitolea kurekodi Filamu ya The Royal Tour kwa lengo la kuhamasisha watalii wa ndani na nje ya nchi kutembelea vivutio vya utalii vya Tanzania na hivyo Watanzania wanatakiwa kumuunga mkono.

Alisema Tanzania ina maeneo mengi yenye vivutio vya utalii ambavyo Watanzania wakitembelea wanaweza wakafurahia, kujifunza na hata kufanya kama sehemu za mapumziko.

Alisema Hifadhi ya Kitulo ina vivutio mbalimbali yakiwamo maua, maporomoko ya maji, ndege na baadhi ya wanyama wanaovutia na kwamba watalii wakitembelea wanaweza wakajifunza na kufurahia.

"Nimekuja huku kwa nia moja tu ya kuhamasisha Watanzania kutembelea vivutio vyetu, nipo na kampeni maalumu ijulikanayo kama 'Talii na Mama Samia' kampeni hii imenileta hapa kwa lengo la kuhamasisha utalii," alisema Nangasu.

Kaimu Ofisa Utalii wa Kitulo, Victor Ramsey alisema kwa sasa watalii wamekuwa wakiongezeka katika hifadhi hiyo kutokana na kuwekwa mazingira rafiki pamoja na kuitangaza kupitia njia mbalimbali ikiwamo mitandao ya kijamii.

Alisema kwenye hifadhi hiyo wapo ndege ambao huwa wanahama kutoka taifa moja kwenda taifa lingine ikiwamo Australia na kwamba ndege hao huwa wanavutia watalii na watafiti.

Alisema hali ya hewa ya eneo hilo pia ni kivutio cha watalii ambao huwa wanapenda hali ya hewa ya aina hiyo huku akisisitiza kuwa watalii wanaopenda hali hiyo huwa wanatembelea zaidi kuanzia Juni.

"Kwenye hii hifadhi pia kuna wanyama kama pundamilia, swala na mbweha ambao pia huwa wanavutia, kwa hiyo tunawakaribisha watalii kuja kutembelea hifadhi yetu ili wajifunze na kufurahia," alisema Ramsey.

Alisema kwenye hifadhi hiyo kuna maporomoko mengi yanayovutia ikiwamo ya Mwakipembo ambayo alisema yanavutia na kwamba yapo mengine ambayo ni marefu zaidi.

Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ni moja kati ya Hifadhi za Taifa zinazopatikana Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambako Bodi ya Taifa za Utalii kupitia mradi wake wa kuhamasisha utalii kusini (Regrow) inahamasisha watalii kutembelea.



# TIA kuinua elimu ya uhasibu Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema ujio wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) katika visiwa vya Zanzibar, utasaidia kuinua kiwango cha elimu ya uhasibu nchini.

Akizindua kampasi ya saba ya chuo hicho jana, visiwani Zanzibar, alisema, ujio wa chuo hicho utasaidia kukidhi mahitaji ya wataalam hao yaanayoonekana kuwa makubwa nchini.

Alisema kuongezeka kwa mahitaji ya kielimu nchini kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuongezeka taasisi za elimu ya juu Zanzibar na ufunguzi wa tawi hilo umekuja wakati sahihi hasa ukizingatia kuna watumishi wengi wenye vikwazo vya kufuata masomo nje ya Zanzibar.

Aidha alisema hatua hiyo ni ya kupongezwa na itafikia matarajio ya Serikali ya kuongeza wataalamu katika sekta muhimu nchini na serikali ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na taasisi hiyo ili kuona wanatoa wasomi waliokuwa na viwango vizuri.

Aidha Waziri Mkuya aliuomba uongozi wa TIA kufungua kampasi nyingine katika kisiwa cha Pemba ili wananchi walio wengi kufaidika na kada hiyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa (TIA) Profesa William Ballargyo, alipongeza serikali ushirikiano uliokuwepo baina yao na kuahidi kuweka vipaumbele muhimu katika udahili ili kuona wenye sifa wanapata fursa ya kujiunga na kampasi hiyo.

Alisema serikali ya Tanzania imetenga jumla ya shilingi bilioni tatu kupitia wizara ya fedha kwa ajili ya hatua za awali za ujenzi.

Meneja Mmiliki wa Taasisi hiyo, Mhandisi, Masuhuko Nkuba, alisema wanatarajia kujenga majengo yao ya kudumu katika Kijiji cha Nganani Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja, ambapo kwa hatua ya mwanzo wataanza na jengo litakalochukuwa wanafunzi elfu moja.

Taasisi ya uhasibu Tanzania (TIA) kwa sasa inaendesha masomo hayo katika jengo la Thabit Kombo katika masomo mbalimbali yakiwemo uhasibu, ugavi na teknolojia ya habari na manunuzi.

**Aidha Waziri Mkuya aliuomba uongozi wa TIA kufungua kampasi nyingine katika kisiwa cha Pemba ili wananchi walio wengi kufaidika na kada hiyo.**

# Mwinyi awakemea viongozi wanaotumia vibaya madaraka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi amewaonya viongozi wa serikali waliopewa madaraka kuacha kutumia vibaya nafasi zao kwa kusababisha madhara kwa jamii na badala yake kujitathmini na kuhakikisha wanaongoza kwa kufuata misingi ya katiba sheria na utawala bora.

Dk.Mwinyi alisema hayo jana wakati akihutubia katika kilele cha siku ya maadili na utawala bora na haki za binadamu katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil Zanzibar.

Alisema Serikali ya Zanzibar inaongozwa kwa kufuata misingi ya katiba na sheria ambapo inatekeleza mambo yote ya msingi ili kuhakikisha haki za wananchi zinalindwa bila ya uonevu na kuvunjwa.

Alisema wapo viongozi wanaokiuka sheria za uongozi wa umma na kutumia vibaya madaraka waliyopewa na kufanya uonevu pamoja na kutelekeza familia zao.

Alisema taarifa zinaonesha wazi kwamba wizara ya nchi ofisi ya rais tawala za mikoa na idara maalum SMZ inaongoza kwa kuwepo kwa taasisi zinazolalamikiwa kwa matumizi mabaya ya nafasi za madaraka kwa watendaji waliokabidhiwa majukumu.

Alisema Tume ya maadili imepokea malalamiko 19 ya ukiukwaji wa matumizi mabaya ya viongozi wa umma ambapo 15 yanahusiana na viongozi ambao wamekabidhiwa majukumu.

"Watendaji wa serikali wahusika waliotajwa katika kujihusisha na matumizi mabaya ya madaraka wajitathmini wenyewe kwa sababu watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1984 inakataza kabisa matumizi mabaya ya madaraka kwa watendaji wake,"alisema.

Aidha Dk.Mwinyi alisema amefurahishwa na kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na kufanikiwa kuokoa mali zaidi ya Sh.bilioni 2.3.

Alisema kwa mujibu wa Mamlaka ya kupambana na rushwa na uhujumu wa Uchumi (ZAECA) sheria namba tano ya mwaka 2023 pamoja na ripoti ya taasisi hiyo kuanzia mwezi wa Januari hadi Oktoba mwaka huu jumla ya Sh.bilioni 2.3 zimeokolewa.

"Sh. milioni 9.7 zimerudishwa kwa wananchi wakati sh.Bilioni 2.2 zimerudishwa serikalini kwa shughuli mbalimbali na matumizi yake,"alisema.

Hata hivyo alisema jumla ya kesi 509 zinazohusiana na rushwa zimepokelewa katika kipindi hicho ikiwemo 341 zinazohusiana na uhujumu wa uchumi.

Alisema kesi 43 zimefungwa wakati kesi 55 zipo kwa ushauri zaidi huku mashauri 26 yamehamishwa, na mashauri 37 yamepekwa kwa Mkurugenzi wa mashtka DPP na kesi tisa zipo mahakamani wakati tano zimetolewa hukumu na wahusika wake wametiwa hatiani.

Dk.Mwinyi alisema ZAECA kwa sasa ipo katika kufanya uchunguzi wa miradi ya maendeleo ipatayo 49 yenye thamani ya Sh.bilioni 652.2 kwa ajili ya kujuwa thamani halisi ya fedha na mali.

Aidha Dk.Mwinyi aliwageukiya viongozi waliotajwa katika fomu za maadili kuhakikisha wanajaza fomu hizo na kukamilisha mchakato huo kabla ya Desemba 31,mwaka huu na sheria kali zinatuchuliwa kwa watakaokaidi agizo hilo .

Alisema wapo waliojisahau na wengine kuona kwamba hakuna hatua za kisheria zitakazochukuliwa na kusisitiza hakuna atakayesalimika kwa kushindwa kutekeleza matakwa ya kisheria ya maadili ya umma.

Mwenyekiti wa Tume ya maadili na utumishi wa umma Assa Othman Rashid, aliwataka watumishi wa umma kuhakikisha wanakamilisha na kujaza fomu za maadili kabla ya tarehe 31 Disembar mwaka huu.

Alisema hadi kufikiya Desemba 18 mwaka huu ni watumishi 922 waliokamilisha na kujaza fomu za maadili na viongozi , sawa na asilimia 36 waliowasilisha fomu.

Aidha alizitaja baadhi ya changamoto ni kuwepo kwa watendaji wa serikali wanaowatisha wafanyakazi ambao wanaotoa taarifa zinazowahusu viongozi huku wengine wakipewa uhamisho.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, ameipongeza Tume ya maadili ya utumishi kwa kutoa elimu kwa viongozi na watendaji wa serikali pamoja na wananchi kwa ujumla hatua ambayo imeleta mafanikio makubwa.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, akizungumza jana katika maonesho ya mavazi ya Wiki ya Mafunzo ya Amali yaliofanyika viwanja vya Mapinduzi Square, Michenzani Mjini Unguja. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Ugumu wa maisha chanzo cha udhalilishaji wanawake, watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Elimu wa Wilaya ya Kati Unguja, Somoe Said Mussa ameiasa jamii kutotumia changamoto ya ugumu wa maisha kama njia ya kudhalilisha wanawake na watoto.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wazazi wa shehia nne za Wilaya ya Kati Unguja, wakati wa mafunzo ya jinsia yaliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA) chini ya ufadhili wa Korea Food for the Hungary International (KFHI).

Alisema hivi sasa watoto wengi wametelekezwa na hukosa malezi ya baba zao kwa kuwa wengi wanakwepa majukumu yao katika malezi kwa familia wakati mtoto anahitaji malezi ya wazazi wake wawili.

Ofisa huyo alisema kutokana na changamoto hiyo imepelekea watoto wengi kufanyiwa udhalilishaji na kushindwa kufikia ndoto za maisha na kuingia katika makundi maovu na biashara ili kupata fedha ya kujikimu.

Alisema serikali na taasisi mbalimbali zipo mstari wa mbele katika kupinga udhalilishaji kwa wanawake na watoto lakini tatizo kubwa lililopo ni kukosekana kwa malezi shirikishi ndani ya jamii.

Ofisa Huduma kutoka Idara ya Elimu Sekondari Khadija Salum, alisema wazazi na walimu wanajukumu kubwa la kumlea mtoto katika malezi bora lakini kuna changamoto kubwa kwa wazazi kutoa ushirikiano hasa muda ambao mtoto yupo shule.

Alisema maendeleo ya teknolojia nayo pia ni sababu ya kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji dhidi ya watoto hivyo elimu ya jinsia inahitajika kutolewa kwa jamii ili kuhakikisha watoto wanapata haki zao zinazostahiki.

Mmoja wa wazazi waliopatiwa mafunzo hayo ,Ali Yussuf, alisema wazazi wanawake ndiyo wahanga wakubwa katika malezi ya watoto na miongoni mwa sababu za akina baba kutojali malezi ya watoto ni ugumu wa maisha.

Ofisa jinsia kutoka shirika linalotekeleza mradi wa kuimarisha mazingira ya elimu kwa mtoto wa kike kumaliza masomo yake, Rosemary Mfui alisema malengo ya mradi huo ni kuona mtoto wa kike anasoma bila ya kuwepo kwa changamoto.

Alisema bado wataendelea kushirikiana na serikali ya Zanzibar katika kutoa elimu ya stadi ya maisha kwa wanafunzi shuleni ili kubaini viashiria vya udhalilishaji na kuepukana navyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOEL ERINEST NDOSSI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 231 TUY Toyota Staut Chassis Namba YK1100003774, Engine Namba 4Y022068. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi Taarifa:

**PHQ/KIL/SAM/6400/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAMECK JAMES AGWANDA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 650 AES – TOYOTA TERCEL. Chassis namba EL517014381. Engine namba 4E1463663. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:

**PHQ/MAR/ROR/2426/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZAHOR MOHAMMED ISSA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 415 CCK – MITSUBISHI CANTER. Chassis namba FE63EGY560021. Engine namba 4D3582105. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:

**PHQ/MAR/TAR/2455/2023.**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 169/2023**

**DICKSON PIUS NDUNGURU -------- MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **REHEMA KOMBA**
2. **ZAMDA MCHEKANAE ----- WAJIBU MAOMBI**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

Mjibu Maombi wa Kwanza unataarifiwa kuwa Mwombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 02/01/2024 saa 2: 30 asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 08/12/2023.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE JUVENILE COURT OF GEITA AT GEITA**

**MISC. CIVIL APPLICATION No. 20 of 2023**

**IBRAHIM SANGA..................APPLICANT**

**VERSUS**

**AGNESS MWAKIPESILE...............RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE THAT,** the above case has been fixed for Mention on the 09th day of January 2024 at 08:00 am.

**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**GIVEN** under my **HAND** and the **SEAL** of the court this 19th day of December, 2023.

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26469/ 2023**

**In the matter of the Estate of the late ELIZABETH MABAI ULAYA of Kitenge within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY KHERI ALPHANI ULAYA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of January, 2024

Dated at Dodoma this 24 Day of November, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26468/2023**

**In the matter of the Estate of the late GEORGE ZEBEDAYO KONYANZA of Chamwino within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY GEMA ZEBEDAYO KONYANZA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 9th Day of January, 2024

Dated at Dodoma this 24 Day of November, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 25899 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOSHUA JAMES MAKENE**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARIA JOSHUA MAKENE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above – named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 31 day of 01, 2024.

DATED at DAR ES SALAAM this 27 day of 11, 2023.

Senior Resident Magistrate

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

LEO UCHAGUZI MKUU;

# Wagombea urais 18, yumo mwanamama pekee

**Kinshasa,** DRC

LEO takriban wapigakura milioni 44 Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wanapiga kura kumchagua rais, wabunge wa kitaifa, wa mikoa na madiwani wa manispaa mbalimbali.

Simulizi ya dunia inaangukia kwenye kinyang'anyiro cha urais, ambacho sasa kumebaki idadi ya wagombea 18, wanane wakiwa wamejiengua na kujiunga na walio vigogo kuwaunga mkono. Awali, Tume Huru ya Uchaguzi (CENI) iliwasajili rasmi wagombea urais 26. Kati yao, wanawake walikuwa watatu.

Mvuto unaotawala sasa ni kati ya Rais Felix Tshisekedi anayetetea kiti chake, dhidi ya gavana wa zamani wa mkoa wa utajiri wa madini wa Katanga, Moise Katumbi huku kukiwapo mwanamama pekee aliyebaki kwenye kinyang'anyiro, Marie-Jose Ifoku, katika nchi hiyo yenye raia zaidi ya milioni 100.

Licha ya changamoto ya usambazaji wa vifaa vya kupigia kura, Tume ya Uchaguzi CENI, inasema raia wa DRC watapiga kura kama ilivyopangwa hii leo.

Saa chache kabla ya vituo vya kupigia kura kufunguliwa, msemaji wa CENI, Patrice Nseya Mulela, alisema vifaa vya kupigia kura vinasafirishwa kwenda katika vituo mbalimbali mkoani Kivu Kaskazini, Kivu Kusini na Ituri, kwa msaada wa jeshi la kulinda amani MONUSCO.

**KUPATA MSHINDI**

Matokeo ya awali, yanatarajiwa kutangazwa Desemba 31, mwaka huu, ingawa CENI inaweza kutangaza mapema iwapo mchakato wa kuhesabu na kujumuisha, utakuwa umekamilika.

Mgombea yeyote atakayepata kura nyingi, atatangazwa mshindi. Hakuna duru ya pili na sio lazima mshindi kupata asilimia 50 ya kura.

Mshindi atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano, lakini anaweza kuwania tena kwa muhula wa pili na wa mwisho.

**MAMBO YA MSINGI**

Kuna wagombea 18, wanaotafuta uongozi wa nchi hiyo, akiwamo Rais Felix Tshisekedi, anayetafuta muhula wa pili.

Tshisekedi anakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Moise Katumbi, mfanyabiashara tajiri na Gavana wa zamani wa Jimbo la Katanga.

Mwingine ni mgombea wa mwaka 2018, Martin Fayulu, anayeaminiwa kushinda uchaguzi uliopita, pia ni daktari wa magonjwa ya wanawake na mshindi wa Tuzo ya Nobel, Denis Mukwege.

Marie-Jose Ifoku, mgombea pekee mwanamke aliyebaki ulingoni kutoka orodha ya wenzake watatu waliojitokeza, anawania urais kwa mara ya pili baada ya kuanguka katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2018.

**ILIVYO DRC**

DRC, ni nchi ya pili kwa ukubwa barani Afrika, yenye utajiri mkubwa wa madini kama shaba, dhahabu, Coltan na Cobalt lakini wananchi wake wengi ni maskini.

Ina ukubwa wa kilomita za mraba milioni 2.34, sawa na Ulaya Magharibi.

Ina watu wanaokadiriwa kuwa milioni 100 kutoka makabila 250. Mikoa ya Mashariki, Kivu Kaskazini, Kivu Kusini na Ituri kwa kipindi kirefu imeendelea kuwa na usalama duni kutokana na kuwapo kwa makundi mengi ya waasi.

Kifaransa ndio lugha rasmi. Hata hivyo, lugha zingine zinazozungumzwa ni pamoja na Kikongo, Lingala, Tshiluba na Kiswahili, zinatambuliwa kama lugha za taifa.

Serikali mbili, ziliwahi kuondolewa madarakani na jeshi mwaka 1965 na 1997.

Viongozi wake wawili waliuawa wakiwa madarakani. Patrice Lumumba mwaka 1961 na Laurent-Desire Kabila mwaka 2001.

Mwaka 2018, ilikuwa mara ya kwanza kwa DRC kushuhudia makabidhiano ya madaraka kwa amani, baada ya Felix Tshisekedi kuapishwa na kuchukua hatamu za uongozi kutoka kwa mtangulizi wake Joseph Kabila, baada ya uchaguzi wa urais ambao, hata hivyo kulikuwa na madai ya wizi wa kura. **RFI**

## Baraza la Usalama lakutana tena kuhusu Gaza

**NewYork,** MAREKANI

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC), lilitarajiwa kupiga kura jana.

Kura hiyo ni kuhusu nakala mpya inayotaka kusitishwa kwa haraka na kudumu kwa mapigano, Gaza.

Upigaji kura katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa uliahirishwa, ili kujaribu kuzuia kura nyingine ya turufu ya Marekani, mshirika wa karibu wa Israel.

Rasimu ya azimio awali ilitoa wito wa kusitishwa kwa haraka kwa uhasama, ili kuruhusu misaada ya kibinadamu kufikishwa kwa Wagaza.

Hatua hiyo imekuja baada ya wakuu wa kijasusi wa Marekani na Israel, kukutana na waziri mkuu wa Qatar, ambaye ni mpatanishi na Hamas, kujaribu kuachiliwa kwa mateka zaidi wa Israel.

Huu ni mkutano wa kwanza, unaojulikana tangu kusitishwa kwa usitishaji mapigano kwa wiki moja mwezi uliopita.

Juzi, wazee watatu walionyeshwa kwenye video mpya ya Hamas. Mmoja wao alisema "walikuwa wakiteseka sana", wakiomba Israeli iwarudishe nyumbani.

Jeshi la Israel lilisema kuwa video hiyo ni ya 'kudharauliwa'. **RFI/BBC**

**Huu ni mkutano wa kwanza, unaojulikana tangu kusitishwa kwa usitishaji mapigano kwa wiki moja mwezi uliopita.**



Waokoaji wakiwa katika kijiji cha Caotan eneo la Minhe Hui, Jimbo la Tu Autonomous, jijini Haidong, China eneo lililokumbwa na tetemeko la ardhi jana na kuthibitishwa watu 111 kufariki dunia, ikiwa ni la pili baada ya tetemeko la awali kuua zaidi ya 100 juzi jioni. **PICHA: XINHUA**

# Tetemeko laua zaidi ya watu 100

**Gansu,** CHINA

WATU 111 wameuawa na wengine 220 wamejeruhiwa katika tetemeko la ardhi lililotokea usiku wa kuamkia jana, kaskazini-magharibi mwa Uchina, vyombo vya habari vya serikali vimeripoti.

Tetemeko hilo la kipimo cha 5.9 richta, lilipiga mkoa wa Gansu muda wa saa sita usiku na kuangusha majengo katika eneo hilo na mkoa wa Qinghai upande wa kusini.

Wafanyikazi wa dharura wanastahimili hali ya baridi kali, kujaribu kusaidia watu katika eneo la mwinuko wa juu. Tetemeko la pili lilipiga mkoa jirani wa Xinjiang, saa chache baadaye jana.

Uharibifu uliosababishwa na tetemeko hilo la kipimo cha 5.5 richta, haujabainika.

Rais wa China, Xi Jinping ameamuru juhudi za uokoaji katika Gansu, mojawapo ya mikoa maskini zaidi ya China.

Gansu, iko kati ya nyanda za juu za Tibet na Loess na inapakana na Mongolia.

Tetemeko hilo, lilipiga mkoa unaojisimamia wa Linxia Hui, eneo la kiutawala la Waislamu wa Hui wa China.

Utafiti wa Jiolojia wa Marekani (USGS), ulisema ulikuwa na ukubwa wa 5.9 richta na kina cha 10km (maili sita).

Picha zilionyesha hospitali zikipokea wagonjwa na waokoaji wakitafuta manusura kwenye vifusi vya majengo yaliyoporomoka. **BBC**

# JKT QUEENS, SIMBA QUEENS KUANZA MBIO ZA UBINGWA

**Na Saada Akida**

PAZIA la Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara msimu 2023/24 linafunguliwa leo kwa nyasi za viwanja vinne kuwaka moto katika mikoa mbalimbali nchini.

Bingwa Mtetezi wa ligi hiyo, JKT Queens, atakuwa na kibarua kigumu ugenini dhidi ya wenyeji wao, Bunda Queens katika Uwanja wa Karume mkoani Mara.

Simba Queens ambao ni mabingwa wapya wa Ngao ya Jamii kwa Wanawake, watawakaribisha Ceasiaa Queens ya Iringa, mchezo utakaochezwa katika Uwanja wa Kituo cha Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Kigamboni.

Mchezo mwingine ni Alliance Girls ya Mwanza ikiwakaribisha Geita Gold Queens, Uwanja wa Nyamagana na Fountain Gate Princess wakiwa nyumbani dhidi ya Aman Queens katika dimba la Jamhuri jijini Dodoma.

Makocha wa timu hizo wakizungumza na Nipashe kuelekea michezo yao, Kocha wa Mabingwa Watetezi wa ligi hiyo, Esther Chabruma, alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo kwa kupambana kutafuta matokeo chanya.

"Tumejiandaa vizuri dhidi ya Bunda Queens, hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu wako nyumbani na timu zote tunahitaji kupata matokeo chanya, tunawaheshimu wapinzani wetu na tutacheza kwa tahadhari kubwa," alisema Chabruma.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Simba, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema wako tayari na wamefanyia kazi mapungufu yao na kukiandaa kikosi chao vema kiufundi ili kuvuna alama tatu dhidi ya Ceasiaa Queens.

"Tuko tayari kukabiliana dhidi ya Ceasiaa Queens , tumewahi kukutana nao mara nyingi na kupata ushindi, hatutawadharau, ila tutacheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu ya ubora waliokuwa nao hasa baada ya kuongeza watu katika usajili wao.

"Tumejipanga vizuri, tunahitaji ushindi ili kurejea heshima ya klabu yetu ikiwamo kushinda kila mechi tukianzia na mchezo wa kesho (leo)," alisema Mgosi.

Naye Kocha wa Fountain Gate Princess, Masuod Juma, alisema amejiandaa vizuri na kwamba kazi kubwa iliyopaki ni wachezaji wake kufanya majukumu aliyowapa katika uwanja wa mazoezi kwa kuhamishia uwanjani.




Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mchezo wao wa marudiano Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Medeama ya Ghana, utakaochezwa leo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. Kulia ni beki wa kushoto wa timu hiyo, Nickson Kibabage. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JKU kileleni raundi ya kwanza Z'bar

**Na Hawa Abdallah. ZANZIBAR**

LIGI Kuu ya Zanzibar mzunguko wa kwanza imemalizika hapo jana kwa mechi kati ya Zimamoto dhidi ya Uhamiaji iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1 katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Mau A visiwani hapa huku JKU SC ikimaliza kileleni.

Kwa sasa ligi hiyo inayojumuisha timu 16, inaelekea mapumziko ili kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi pamoja na usajili wa dirisha dogo kwa ajili ya mzunguko wa lala salama, ambao hata hivyo bado Bodi ya Ligi Zanzibar haijatoa taarifa ya lini itaendelea.

Ligi hiyo inakwenda mapumziko huku JKU SC ikiwa kileleni mwa msimamo na alama 36 ikifuatiwa na Zimamoto SC yenye alama 30 na nafasi ya tatu ilishikiliwa na Bingwa Mtetezi, KMKM SC yenye alama 29.

Akizungumzia na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohmed Hilali, alisema katika kipindi hiki cha mapumziko pamoja na usajili atakitumia kufanyia maboresho kikosi chake ili kufanya vizuri mzunguko wa lala salama.

Alisema tayari ametuma mapendekezo yake ya usajili kwa uongozi wa timu hiyo ili kupata wachezaji ambao wataweza kuziba mapengo ambayo yameonekana mzunguko wa kwanza.

Hilali alisema miongoni mwa mapendekezo aliyoyatoa ni kusajili wachezaji sita akiwamo kipa, washambuliaji pamoja na beki wa kushoto idara ambazo makosa mengi yalionekana katika mzunguko wa kwanza.

Kuhusu wachezaji watakaoacha, alisema amepeleka mapendekezo hayo kwa kuwa wapo baadhi viwango vyao haviendani na mikimiki ya Ligi Kuu Zanzibar.

"Lazima tuwe makini na tusifanye makosa katika mzunguko huu wa lala salama, tutumie mzunguko huu kuiboresha timu na kuondoa makosa ambayo tumeyaona, kama tutafanya vizuri na kwa makini basi malengo yetu yatatimia," alisema Hilali

Alisema bado anaendelea na mpango wake wa mbio za ubingwa wa ligi hiyo ambapo bado kuna mchuano mkali kwa timu zilizo katika nafasi tano za juu kutokana na kutopishana kwa alama nyingi katika msimamo.

Hata hivyo, aliuomba uongozi wa Zimamoto SC kuongeza hamasa kubwa katika mzunguko wa pili kama ilivyo kwa timu nyingine ili kuwahamasisha wachezaji kufanya vizuri katika michezo yao.

# Kocha Dodoma Jiji aianika Ihefu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope, amesema ushindi walioupata juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wa bao 1-0 dhidi ya Ihefu FC ulikuwa wa kimbinu zaidi na si uwezo au ufundi wa mchezaji mmoja mmoja kwani mechi ilitawaliwa zaidi na matumizi ya nguvu.

Liogope amesema Ihefu ina timu nzuri, hivyo ilitumika mifumo mitatu ili kupata ushindi wa bao hilo lililofungwa dakika ya 55 na Yassin Mgaza.

"Mpira ulitawaliwa sana na matumizi ya nguvu, Ihefu wana timu nzuri, walianza na mastraika watatu tena wenye nguvu, ndiyo maana sisi tukaanza na viungo wakabaji wawili, halafu tukachezesha straika mmoja, lakini kipindi cha kwanza niliona mabeki wao wako huru sana, baada ya mapumziko nikaongeza mwingine ili kuwafanya wawe bize na kweli ilisababisha tukapata bao.

"Baada ya hapo nikabadilisha tena mfumo ili kulilinda bao, tukapata ushindi, mechi kama hizi unatakiwa kucheza kimbinu na hazina mabao mengi," alisema Liogope.

Kocha Msaidizi wa Ihefu, Themi Felix, aliwapongeza Dodoma Jiji kwa ushindi akisema walitumia nusu nafasi tu ili kupata pointi tatu.

"Tulicheza vizuri, mpango wetu ulikuwa kuwashinikiza wasije kwetu, tulikuwa tunamaliza mechi kipindi cha kwanza tu, tumewakosa sana, wao wamepata nusu nafasi tu wamefunga bao ni kwa sababu washambuliaji wetu hawakuwa makini," alisema.

Ni ushindi uliowapeleka Dodoma Jiji nafasi ya saba ya msimamo ikiwa na pointi 18, Ihefu ikibaki nafasi ya 14 ikiwa na alama 13.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BARCA KUMUUZA RAPHINHA

BARCELONA ipo tayari kupokea ofa ya kumuuza winga wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 27, huku Manchester United ikifikiria kupendekeza mpango wa kubadilishana utakaomhusisha Jadon Sancho. **(Sport)**

### SANTO AWANIWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest inatazamiwa kumteua kocha wa zamani wa Wolves na Tottenham Hotspur, Nuno Espirito Santo siku chache zijazo, ambapo Mreno huyo mwenye umri wa miaka 49, atachukua nafasi ya kocha wa sasa, Steve Cooper. (**A Bola**)

### GUIRASSY LULU ULAYA

KLABU za Manchester United, Fulham, West Ham na AC Milan walikuwa na maskauti kwenye Uwanja wa Allianz Arena Jumapili kumfuatilia mshambuliaji wa Stuttgart na Timu ya Taifa ya Guinea, Serhou Guirassy, wakati wa mechi yao dhidi ya Bayern Munich. **(90 min)**

### DAN ATAJWA MAN UNITED

MKURUGENZI wa Michezo wa Newcastle United, Dan Ashworth, ndiye chaguo kuu la Ineos Group kuchukua nafasi hiyo pale Manchester United. **(Manchester)**

### SPURS YAMFUATA TODIBO

KLABU ya Tottenham Hotspur imefanya mazungumzo juu ya uwezekano wa kumnunua beki wa Nice na Ufaransa, Jean-Clair Todibo, 23. **(Mail)**

### WOLVES KUSAJILI WAWILI

KLABU ya Wolves iko tayari kusajili angalau wachezaji wawili wapya katika dirisha la usajili la Januari. Mshambuliaji wa Viktoria Plzen, Rafiu Durosinmi mwenye umri wa miaka 20 anabakia kuwa mlengwa wao mkuu. **(Telegraph)**

### ADAMS NA FULHAM

KLABU ya Fulham inatathmini dau la Januari kwa mshambuliaji wa Montpellier mwenye umri wa miaka 23 kutoka Nigeria, Akor Adams. **(Football Insider)**

### LENGLET KUPELEKWA SOKONI

BARCELONA inaweza kusitisha mkopo wa Clement Lenglet kule Aston Villa katika dirisha la uhamisho la Januari na kisha kujaribu kumuuza beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 28, huku AC Milan ikimtaka. (**Football Insider**)

### MAATSEN KUPIGWA BEI

CHELSEA ipo tayari kumuuza beki wao, Ian Maatsen katika dirisha la Januari, huku Manchester City, West Ham, Borussia Dortmund, Napoli na Roma zikitaka huduma za Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 21. **(90 min)**

### MADUEKE HATARUHUSIWA

CHELSEA haina nia ya kumruhusu winga Mwingereza Noni Madueke mwenye umri wa miaka 21, kuondoka kwa mkopo Januari. **(Athletic)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VARANE AIGANDA UNITED

## Ataka kuongeza mwaka, lakini klabu hiyo haina nia ya kuwezesha chaguo hilo...

**MANCHESTER, England**

RAPHAEL Varane ameripotiwa kutaka kuongeza mkataba wake Manchester United, huku beki huyo wa Ufaransa akilazimika kurejea kwenye kikosi.

Varane alianza mechi yake ya nane msimu huu kwa 'Mashetani Wekundu' hao katika suluhu na Liverpool Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, alishirikiana na Jonny Evans katika safu ya ulinzi ya Man United wakati wakiondoka na pointi moja pale kwenye dimba la Anfield.

Varane amelazimika kurejea katika kikosi cha Kocha Erik ten Hag huku kukiwa na tatizo la safu ya ulinzi.

Kuanza kwake wiki iliyopita dhidi ya Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ilikuwa ni mara ya kwanza kwake ndani ya wiki saba.

Kwa mujibu wa gazeti la Manchester Evening News, Varane bado ana nia ya kubaki Old Trafford licha ya kuwa amecheza mechi 14 katika michuano yote msimu huu.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ligi ya Mabingwa Ulaya, alisajiliwa na United kutoka Real Madrid msimu wa majira ya joto wa 2021 kwa mkataba wa pauni milioni 42.

Awali, Varane alitangazwa kusaini mkataba wa miaka minne, lakini baadaye ikabainika kuwa mkataba wake ulikuwa wa miaka mitatu ya awali na chaguo la kuongeza mwaka mmoja.

Beki huyo wa kati anaripotiwa kuwa na matumaini ya kuamsha nyongeza ya mwaka mmoja katika mkataba wake, ambao utaongeza muda wake wa kukaa hadi msimu wa majira ya joto wa 2025.


Ripoti zilidai wiki iliyopita kwamba United haina nia ya kuwezesha chaguo hilo, na hivyo kufungua mlango kwa Varane kuondoka kama mchezaji huru msimu wa majira ya joto.

Wachezaji ambao wanaingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wao wanaruhusiwa kukubaliana na klabu nyingine katika dirisha lijalo la usajili la Januari.

Varane alikuwa tegemeo katika safu ya ulinzi ya United msimu uliopita kwa ushirikiano wake pamoja na Lisandro Martinez.

Hata hivyo, jeraha la muda mrefu kwa Martinez limemfanya Varane kutatizika na kuwa chaguo la pili mbele ya Harry Maguire na Jonny Evans.

# MOURINHO AFICHUA TATIZO MAN UNITED



**ROME, Italia**

JOSE Mourinho amesema aliiambia Manchester United kwamba hawataweza kufanikiwa kwa sababu ya baadhi ya wachezaji na wafanyakazi ambao wapo katika klabu hiyo wakati akiwa pale.

Mourinho aliiongoza United kutoka mwaka 2016 hadi 2018, akishinda Ligi ya Europa na Kombe la Carabao katika msimu wake wa kwanza na kumaliza wa pili mbele ya Manchester City msimu wa 2017-18.

"Bado kuna watu katika klabu hiyo, na ninaposema watu namaanisha wachezaji fulani lakini pia watu wengine ambao si wachezaji, ambao bado wapo nilipoiambia (United): Ukiwa na watu hawa, hautawahi kufanikiwa na bado wapo," alisema Mourinho akiiambia Podcast ya Obi One ya John Obi Mikel.

"Nikiwa Man United, nilibadilisha mchezaji wakati wa mapumziko... wakala wake alikuwa akinishutumu kwa uonevu.

"Nililazimika kubadilika. Nakumbuka nyakati hizi, na ninacheka kuhusu nyakati hizi, lakini ni nyakati tofauti."

Roma wako katika nafasi ya saba kwenye Serie A baada ya Jumapili kufungwa mabao 2-0 na Bologna ya Thiago Motta - lakini Mourinho alisema angependa kuendelea na kazi yake katika mji mkuu wa Italia baada ya mwisho wa mkataba wake Juni 2024.

"Nimechanganyikiwa na mambo mengi - lakini hakuna hata moja kati ya hayo yenye nguvu kuliko hisia zangu za ukaribu na klabu hii," alisema Mourinho.

"Nikiondoka mwisho wa msimu hautakuwa uamuzi wangu, nataka niendelee hapa na nasema hivi kwa sababu wakati mwingine ni bora kuwa wazi.

"Ikiwa hatuwezi kusajili wachezaji wa juu, kama (Romelu) Lukaku kwa mfano, ni bora kufanya kazi na wachezaji wachanga kuliko watu ambao hawakupi chochote."

# Barca kusajili kiungo Januari

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amesema klabu hiyo itatafuta kiungo wa kati Januari kwa mkataba sawa na ule uliomleta Edgar Davids katika klabu hiyo mwaka 2004.

Davids alijiunga na Barca kwa mkopo katikati ya kampeni ya msimu wa 2003-04 walipokuwa nafasi ya saba kwenye msimamo na kusaidia kumaliza nafasi ya pili.

Huku Gavi akiwa majeruhi hadi mwisho wa msimu, Laporta amesema Barça itatafuta mchezaji kama huyo Januari.

"Ikiwa tutafaulu kufanya mchezo wa haki ufanyike na LaLiga, wazo ni kuwa na kiungo mwingine wa kufidia hasara ya Gavi," alisema Laporta akiiambia EFE.

"Itakuwa mkopo hadi mwisho wa msimu, kama tulivyofanya miaka iliyopita na Edgar Davids, kwa mfano. Nafikiri kabla ya mwisho wa mwaka tunaweza kutengeneza nafasi ya mikataba kadhaa tunayofanyia kazi."

ESPN ilifichua Oktoba kwamba Barca wanataka kusajili kiungo mwingine ili kuunda ushindani kwa Oriol Romeu, ambaye alijiunga nao msimu uliopita wa majira ya joto kama mbadala wa Sergio Busquets.

Mpango wa awali ulikuwa wa kuwekeza katika majira ya joto yajayo, lakini jeraha kwa Gavi, ambalo lilimpata akiwa kwenye majukumu ya kimataifa na Hispania Novemba, limewalazimu kubadili mipango yao.

FIFA itafidia Barca kwa kuumia kwa Gavi, ambaye atakuwa nje hadi miezi 10, wakati LaLiga itawapa nafasi ndani ya ligi iliyopangwa kusajili mbadala wake.

Hata hivyo, matatizo ya kifedha ya klabu hiyo yanamaanisha kuwa watalazimika kutafuta soko la mkopo, kama walivyofanya kwa Davids takriban miaka 20 iliyopita. Mholanzi huyo aliondoka baada ya miezi sita tu katika klabu hiyo kwani uhamisho wa kudumu haukuweza kuafikiwa.

Barca pia itamleta mshambuliaji wa Athletico, Paranaense Vitor Roque mwezi ujao. Mbrazil huyo atawasili kwa kitita cha euro milioni 30 na nyongeza ya euro milioni 31.

## Fluminense yatinga fainali Klabu Bingwa ya Dunia

**JEDDAH, Saudi Arabia**

JOHN Arias na John Kennedy walifunga katika kipindi cha pili na kuipa timu ya Fluminense ya Brazil ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Al-Ahly ya Misri katika nusu fainali ya Klabu Bingwa ya Dunia kwenye Uwanja wa King Abdullah Sports City mjini Jeddah Jumatatu.

Wakifundishwa na kocha wa muda wa Brazil, Fernando Diniz, mabingwa hao wa Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini), watakabiliana na mshindi kati ya Manchester City na Urawa Red Diamonds ya Japan katika fainali Ijumaa mjini Jeddah.

Arias alifunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 71 baada ya beki wa zamani wa Real Madrid, Marcelo, kufanyiwa madhambi ndani ya eneo la hatari.

"Siku zote mimi hujaribu kufanya kitu tofauti. Siku zote nimejaribu katika maisha yangu yote," alisema Marcelo akiiambia Globo.

"Wakati huo, mchezo ulikuwa wa mwisho. Sikufikiria hata kupiga chenga ili niingie ndani ya eneo hilo.


"Kwa hiyo nilifanikiwa kufika mbele yake na akanifanyia faulo. Haikufikiriwa, ilikuja papohapo na ilikuwa nzuri."

Mchezaji wa akiba Kennedy aliongeza la pili dakika ya 89 na mkwaju mkali akimaliza shambulio la kushtukiza.

Wakati Marcelo alisaidia kuunda Bingwa wa Amerika Kusini kwa upande mmoja, mlinzi Felipe Melo mwenye umri wa miaka 40 na kipa Fabio mwenye umri wa miaka 43, walilinda upande mwingine.

Felipe Melo alitengeneza wakati mzuri katika kipindi cha kwanza, akikimbia kuelekea langoni kumkaba Percy Tau, ambaye alikuwa tayari kupiga shuti.

Utulivu wa Fabio na hisia sahihi za kukaa kwenye nafasi zilimruhusu kuokoa mara kwa mara kutoka majaribio 18 ya Al Ahly.



HABARI MICHEZO

# BANDA KUTUA SINGIDA FG KWA SH. MILIONI 200

**Na Saada Akida**

WAKATI Singida Fountain Gate FC, wamefungiwa na Shirikisho la Soka Ulimwenguni (Fifa), kutofanya usajili hadi wamlipe aliyekuwa beki wao, Pascal Wawa, timu hiyo inahusishwa na kumsajili aliyekuwa mchezaji wa zamani wa Simba, winga Mmalawi Peter Banda.

Taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jana, Banda anatarajiwa kujiunga na Singida mapema mwezi huu baada ya makubaliano ya mkataba wa miaka miwili katika usajili ya dirisha dogo lililofunguliwa wiki iliyopita.

Mtoa habari huyo alisema nyota huyo atasaini mkataba huo kwa Dola za Marekani 80,000 zaidi ya Sh. milioni 200 za Tanzania, kwa kulipwa kwa awamu mbili na muda wowote wanaweza kumalizana naye.

"Ni kweli tumeingia katika makubaliano na baadhi ya wachezaji akiwamo Banda, tunatarajia kufanya usajili mzuri kuimarisha kikosi chetu, lakini kwa sasa tuko kwenye adhabu, nina imani hiyo itapita na kuruhusiwa kusajili," alisema mtoa habari huyo.

Nipashe lilimtafuta Msemaji wa Singida Fountain Gate FC, Hussein Masanza, ambaye alisema kwa sasa hawawezi kufanya usajili kwa sababu wamefungiwa na Fifa kwa kosa la kuchelewesha malipo ya Wawa.

"Kwa sasa ni ngumu kuweka wazi kuhusu suala la usajili, kwa sababu tupo kwenye adhabu ya kutosajili hadi tutakapomaliza kumlipa aliyekuwa beki wetu, Wawa, ambaye tuliachana naye mwanzoni mwa msimu huu," alisema Masanza.

Naye Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema hawajapata taarifa yoyote kutoka Fifa juu ya kufunguliwa usajili kwa Singida Fountain Gate FC.

"Ni kweli Singida Fountain Gate FC wako kwenye adhabu ya kutosajili hadi wamlipe aliyekuwa mchezaji wao wa zamani, Wawa, hivyo kama watafunguliwa basi Fifa watatoa taarifa kama ilivyo kwa Simba na Yanga walifungiwa baada ya kuwalipa waliokuwa wanawadai," alisema Ndimbo.

SAMBARATISHA...




Beki wa Simba, Henock Inonga, akiambaa na mpira katikati ya wachezaji wa Wydad ya Morocco, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, ambayo walishinda 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# SIMBA WAWAWAAAH!

INATOKA UK. 24

wachezaji wengi viungo wa uchezeshaji na kuwaingiza mabeki, huku wakionekana baadhi ya wachezaji ambao hawajawahi kuonekana uwanjani.

Wachezaji kama David Kameta ,Duchu' na Abdallah Hamisi walionekana kwa mara ya kwanza wakiichezea Simba tangu wasajiliwe msimu huu, huku pia akiingia Israel Mwenda, Kennedy Juma, lakini akiwatoa kina Chama, Onana na Kibu, huku Mohamed Hussein, Shomari Kapombe, Henock Inonga bado wakiwa uwanjani.

Ni kipindi ambacho Simba ilifanya mashambulizi machache, lakini ya hatari kwenye lango la wapinzani hao, huku Wydad Casablanca ikihamia langoni mwa wenyeji wao dakika 10 zote za mwisho wa mchezo na nane za nyongeza, ambapo kazi ya wachezaji wa ,Wekundu wa Msimbazi' ilikuwa ni kuokoa na kulinda ushindi walioupata kipindi cha kwanza.

Kwa matokeo hayo, Wydad Casablanca inarejea mkiani, ikibaki na pointi tatu ilizozipata kwa kuifunga Simba bao 1-0 mechi iliyopita, Desemba 9 nchini Morocco.

Simba sasa italazimika kufanya vizuri kwenye mechi zake mbili zitakazochezwa Februari 23 ugenini dhidi ya Asec Mimosas na ya Machi Mosi mwakani, Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Jwaneng Galaxy.

### HALI ILIVYOKUWA

Baada ya bao la pili lililofungwa na Onana, liliwachukiza mashabiki wa Wydad Casablanca na kutaka kutoka uwanjani lakini baadhi ya mashabiki wa Simba upande wa kusini mwa uwanja waliwazuia na kuwataka kubaki hadi mwisho wa mechi.

### MILIONI 10 BAO LA MAMA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, baada ya mechi hiyo aliwakabidhi wachezaji wa Simba Sh. milioni 10 ikiwa ni ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kununua kila bao la ushindi kwa Sh. milioni tano kwa wawakilishi hao wa Tanzania kwenye mechi za kimataifa.

Fedha hizo zilikabidhiwa mbele ya Naibu wa Wizara hiyo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA.

„Moja ya vitu vinaniburudisha ni viwango vya timu zetu zinafurahisha sana, mambo mengi na uwekezaji ambao wanaofanya unaboresha timu zao, kwa hali hiyo ,Bao la Mama' litaendelea kutolewa.

„Serikali kazi yetu ni mmoja, kuhakikisha hatukwamishi klabu zetu kufikia malengo, matumaini yetu na Yanga itafanya vizuri katika mchezo wao wa kesho (leo)," alisema Mwana FA.

## Gamondi: Ni ushindi tu leo

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kusaka pointi tatu muhimu zitakazowaweka katika mbio nzuri za kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, amesema "kundi letu ni gumu kutokana na timu tulizopangwa nazo ila tumejipanga kushinda mchezo wa leo dhidi ya Medeama".

Yanga ambayo inaburuza mkia katika Kundi D ikiwa na pointi mbili, kama itashinda mchezo huo, itafikisha alama tano kama kinara wa kundi hilo, Al Ahly ambayo jana haikucheza dhidi ya Belouizdad kutokana na kuwa kwenye fainali za Klabu Bingwa Dunia.

Katika kundi hilo, Belouizdad inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi nne sawa na Medeama, hivyo nalo bado lipo wazi kwa timu yoyote kuweza kufuzu robo fainali.

Gamondi alisema mchezo huo wanahitaji kucheza kwa akili ili kupata ushindi, ingawa anajua hautakuwa rahisi kwa sababu kila mmoja anahitaji pointi muhimu ikiwamo wageni wao hao.

"Kesho ni mchezo mgumu wa kutumia akili, kucheza vizuri zaidi na kutumia nafasi tunazotengeneza na kutumia makosa ya wapinzani wetu," alisema Gamondi.

Kwa upande wa Mchezaji wa Yanga, Nickson Kibabage, alisema wao kama wachezaji wana morali kuelekea katika mchezo huo, ili kupata matokeo ambayo yatawafanya kuwa na nafasi ya kusonga mbele.

Kocha wa Medeama FC, Evans Augustine Adotey, alisema wamefurahi kwa mapokezi mazuri na amejiandaa kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri dhidi ya Yanga.

Alisema ameandaa wachezaji wake kisaikolojia na amekuja na mipango yao ya kwanza ni kuvuna alama tatu ikishindikana basi watafute pointi moja dhidi ya wapinzani wao, Yanga.

"Sijapata muda mzuri wa maandalizi ya kikosi changu, lakini nimejipanga kushinda mchezo huo na kusonga mbele na kwenda kucheza robo fainali," alisema.

Nahodha wa Medeama FC, Baba Abdulai Musah, alisema wako vizuri kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri ambayo watarudi nayo nyumbani.

Alisema licha ya Yanga kuwa mbele ya mashabiki wengi, lakini wao wako 11 na wapinzani wao 11 uwanjani, hivyo anaamini utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa.



# Michezo

Jumatano Desemba 20, 2023

Nipashe





## Gamondi: Ni ushindi tu leo

UKURASA 23




Mfungaji wa mabao mawili ya Simba, Willy Onana, akishangilia moja ya mabao yake kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad ya Morocco iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, ambayo walishinda 2-0. Kushoto ni mashabiki wa timu hiyo wakishangilia. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# SIMBA WAWAWAAAH!

## Mwamba Onana ang'ara akiisafishia njia robo fainali CAF, Kipa Lakred aikwamisha Wydad...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABAO mawili ya Mcameroon Willy Onana, jana yalifufua matumaini ya Simba kutinga kwa mara nyingine tena robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikishinda 2-0 dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ushindi huo umeipeleka Simba kwenye nafasi ya pili ya Kundi B ikifikisha pointi tano, nyuma ya Asec Mimosas ya Ivory Coast inayoongoza ikiwa na pointi saba kabla ya mchezo wao wa jana usiku dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana iliyokuwa na pointi nne.

Onana alifunga bao la kwanza dakika ya 36, baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Fabrice Ngoma aliyeupata mpira katikati ya uwanja na kuupiga mbele kwa Jean Baleke ambaye aliamua kupiga shuti lililowababatiza mabeki wa Wydad Casablanca, mpira ukamkuta Kibu Denis aliyekuwa mbele kidogo, akaurudisha nyuma kwa mfungaji ambaye alikuwa ndani kidogo ya eneo la hatari, akapiga shuti kwa mguu wa kulia ambalo kipa Youssef El Motie hakuliona.

Dakika mbili baadaye, winga huyo ambaye hakuanza vizuri msimu na mara kwa mara akilaumiwa na mashabiki wa Simba kuwa anacheza mpira laini na wa kwenye majukwaa zaidi kuliko kuisaidia timu, alipachika bao la pili.

Bao hilo lilianzia kwa kipa Ayoub Lakred ambaye aliurusha mpira mrefu hadi katikati ya uwanja, pembeni kwa Clatous Chama ambaye aliamba nao na kuwahadaa mabeki wa wageni, akauingiza ndani kwa Onana aliyemrudishia tena Chama na yeye akatoka mbio kutafuta chumba. Chama akamrudishia tena, hakufanya ajizi, akauweka tena wavuni kwa mguu wake wa kulia.

Mpira ulianza taratibu ambapo wageni walionekana kutawala zaidi na kuwabana kwa kuwachezea nusu uwanja, huku Simba ikionekana kama vile kuwasoma wapinzani wao.

Onana alianza kuonesha machachari yake mapema tu dakika ya tisa baada ya kuwahadaa mabeki wa Wydad Casablanca na kupiga shuti ambalo lilidakwa vema na kipa Youssef El Motie.

Wageni walijibu kwa shambulizi kali dakika ya 12, wakati mchezaji Montasser Lahtimi alipowatoka mabeki wa Simba, lakini shuti lake lilienda nje ya lango.

Mzamiru Yassin aliikosesha Simba bao dakika ya 22, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Baleke, lakini wakati akijivuta na kujishauri kutaka kupiga, uliokolewa na Amine Aboulfath.

Bouly Sambou, nusura aipatie bao timu yake ya Wydad Casablanca dakika ya 27, alipoachia shuti kali la kushtukiza akiwa umbali wa mita 30, lakini shuti lake lilitoka juu kidogo ya lango la Simba.

Kipa, Lakred alifanya kazi ya ziada dakika ya 28, alipookoa mara mbili, mashuti ya Sambou ambaye alipiga shuti lililopanguliwa na kipa huyo, kabla ya kumkuta Lahtimi ambaye alipiga tena na kipa akaupangua na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Dakika nne baadaye, Lakred aliiokoa tena Simba isifungwe alipodaka kwa ustadi shuti la Zakaria Draoui na hadi mapumziko Simba ilikuwa inaongoza kwa mabao 2-0.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, lakini Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha aliwashangaza wengi, alipowatoa

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >